Haliuzwi
APRIL 27, 2026
/islamicftz
Dhul-Qadah 10 1447
IMAAN
ISSN 5618 - NO. 581
Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah



## Mahujaji waanza safari kwa imani inayoshinda hofu ya vita

# CIFCA: Itungwe sheria ya fedha za Kiislamu

Licha ya kuwepo kwa miongozo ya Takaful, Sukuk na benki, Mwenyekiti wa CIFCA, Aref Nahdi, ameomba Serikali kutunga sheria pana itakayotawala juu ya miongozo iliyopo ya huduma ya fedha za Kiislamu



Mwenyekiti wa The Islamic Foundation, Aref Nahdi (kulia), akiwa na Wakili wa Serikali kutoka Tume ya Kurekebisha Sheria iliyo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria, Baraka Chipandu aliyetembea vyombo vya habari vya Imaan, mjini Morogoro, kwa ajili ya kutoa elimu.


**AlHuda CIBE yashirikiana na AIID kuendeleza fedha za Kiislamu Afrika**

## Baytulmaal yagawa Sh milioni 50 kusaidia wahitaji 100 Dar

- Ni kwa ajili ya Zaka kwa wanufaika 100, ikiwa ni sehemu ya juhudi za kupunguza umasikini na kuwawezesha wananchi kiuchumi



## Rais Mwinyi ataka misikiti kuwa chachu ya suluhu za kijamii



## Saudi yazindua mfumo wa kidijitali kufuatilia msongamano Msikiti Mkuu

NA MWANDISHI WETU

# Mwenyekiti CIFCA ataka huduma za fedha za Kiislamu zitungiwe sheria

**Aref Nahdi, akitaja moja ya hasara ya kukosekana kwa sheria, alisema, kwa sasa kukitokea kusigana kwa aina yoyote katika miongozo iliyopo ya huduma hizo, hakuna kimbilio kwa sababu hakuna sheria kuu (regulatory framework) ambayo inaongoza sekta hiyo.**

Licha ya uwepo wa miongozo ya kisheria ya sekta mahsusi za huduma za fedha za Kiislamu kama Takaful, Sukuk na Benki; Mwenyekiti wa Kituo cha Huduma za Kifedha za Kiislamu na Ushauri Tanzania (CIFCA), Aref Nahdi, ameiomba Serikali ihitimishe uhitaji kwa kutunga sheria pana ya sekta nzima.

Nahdi alitoa ushauri huo ofisini kwake katika mazungumzo mafupi na Wakili wa Serikali kutoka Tume ya Kurekebisha Sheria iliyo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria, Baraka Chipandu aliyetembea vyombo vya habari vya Imaan, mjini Morogoro, kwa ajili ya kutoa elimu.

Nahdi, ambaye pia ni Mwenyekiti wa taasisi ya The Islamic Foundation inayomiliki vyombo vya habari vya Imaan, alimwambia Wakili Chipandu kuwa faida nyingi zitapatikana kukiwepo na sheria itakayotawala juu ya miongozo iliyopo sasa kwenye matawi ya sekta hiyo pana.

"Kwenu nyinyi, Tume ya Kurekebisha Sheria, mnajua kuwa kunakuwa na sheria halafu miongozi inaelekeza katika namna ya utekelezaji wa hiyo sheria. Sasa, sisi tuna miongozo isiyo na sheria, jambo ambalo halipo sawa," alisema Nahdi.


Baadhi ya miongozo ya sekta mahsusi za huduma za fedha za Kiislamu iliyopo tayari ni pamoja na Miongozo ya Bima yenye kufuata misingi ya dini ya Kiislamu (TAKAFUL) iliyotolewa mwaka 2022 na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA); Miongozo ya Sukuk iliyotolewa mwaka 2023 na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA); na Miongozo ya Kanuni za Benki na Taasisi za Fedha (Biashara ya Benki Isiyotumia Riba) ya 2025 iliyotolewa na Benki Kuu.

Aref Nahdi, akitaja moja ya hasara ya kukosekana kwa sheria, alisema, kwa sasa kukitokea kusigana kwa aina yoyote katika miongozo iliyopo ya huduma hizo, hakuna kimbilio kwa sababu hakuna sheria kuu (regulatory framework) ambayo inaongoza sekta hiyo.

"Na hii inakwenda pia katika masuala mazima ya kodi na kadhalika. Miamala mingi ya fedha ya Kiislamu inakuwa inalipishwa kodi zaidi ya mara moja kwa sababu katika miamala ya kawaida, kwa mfano ya benki, kuna sheria ya kodi, sheria ya fedha; lakini huku hakuna sheria ya huduma za benki za Kiislamu," alisema.

Kwa kipindi chote tangu huduma za fedha za Kiislamu zilipoingia hapa nhini, zikitanguliwa na benki za Kiislamu kwa ujio wa KCB mwaka 2008, kilio cha wadau kimekuwa ni kukosekana kwa sharia ingawa kwa sasa nafuu imepatikana kwa walau kuwepo miongozo ya sekta ndogo ndogo chini huduma za fedha za Kiislamu.

Baada ya kutambulishwa kwa KCB inayotoa huduma kupitia dirisha la Kiislamu, benki nyingine kadhaa zimefuata nyayo zikiwemo NBC, PBZ, CRDB na CRDB ambayo ndio pekee benki kamili ya Kiislamu. Kadhalika, ukiacha huduma benki, kuna huduma za bima ya Kiislamu na Sukuk, maarufu kama hatifungani ya Kiislamu.



HABARI
DAR ES SALAAM

NA MWANDISHI WETU



# Baytulmaal yagawa Sh milioni 50 kusaidia wahitaji 100 Dar

Baytulmaal Tanzania imetoa jumla ya Shilingi milioni 50 za zaka kwa wanufaika 100 katika tukio lililofanyika Msikiti wa Kisumu, Magomeni Mikumi jijini Dar es Salaam, ikiwa ni sehemu ya juhudi za kupunguza umasikini na kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Wanufaika wa mgao huo wanajumuisha wajasiriamali wadogo, hususan waliokumbwa na janga la kuungua vibanda katika soko la Ubungo Mawasiliano, familia zilizoathirika na mvua katika kijiji cha Doda wilayani Mkinga mkoani Tanga, pamoja na makundi mengine yenye uhitaji maalum kama wagonjwa, wanafunzi, wafungwa na watu wenye madeni.

Akizungumza katika halfa hiyo, Katibu wa Baitulmaal Tanzania, Haji Mrisho Rubibi, amesema wengi kati ya wanufaika ni wanawake wajane na kwamba uamuzi wa kuwapendelea zaidi ni wa makusudi kwa sababu, aghlab, nyuma yao kuna yatima wanaowategemea. Mnufaika, Ashura Haruna, mmoja wa walioungulіwa na mabanda yao katika soko la Ubungo Mawasiliano mwanzoni mwa mwezi huu, amesema zaka aliyopokea, itamuwezesha kuanza upya katika biashara yake.

Taasisi ya Baitulmaal, iliyoanzishwa mwaka 2002 kwa lengo la kukusanya na kugawa zaka, imeendelea kuimarisha shughuli zake, hasa baada ya kupata msukumo mpya mwaka 2022. Tangu kipindi hicho, Baytulmaal imefanikiwa kukusanya zaidi ya Shilingi milioni 120 na kuzigawa kwa wahitaji wanaostahiki.

Mbali na kutekeleza wajibu wa kidini, Mwenyekiti wa bodi ya taasisi hiyo, Sheikh Dkt Ibrahim Ghulam, ameeleza kuwa shughuli za Baytulmaal zina mchango mpana katika juhudi za kitaifa za kupunguza umasikini. Alisema kupitia uwezeshaji wa mitaji kwa watu wa kipato cha chini, taasisi hiyo inasaidia kukuza biashara ndogo ndogo, kuimarisha uchumi wa wananchi na kuongeza mshikamano wa kijamii.

Baytulmaal Tanzania inasimamiwa kwa pamoja na Bodi ya wataalamu na wanazuoni wa Kiislamu chini ya ulezi wa Jumuiya ya Wataalamu wa Kiislamu Tanzania (TAMPRO) pamoja na Umoja wa Wanazuoni Tanzania (Hay'atul Ulamaa).

Mwenyekiti na Katibu wake, wote walirejea wito kwa watu wenye uwezo na vipato kulipa zaka kupitia taasisi hiyo ili kusaidia kuwainua wahitaji na kupunguza changamoto za kiuchumi katika jamii.

Aidha Dkt Ghulam na Rubibi, walizihimiza kampuni na taasisi mbalimbali kushirikiana na Baytulmaal katika ukusanyaji na ugawaji wa zaka ili kufanikisha kuwafikia walengwa wengi zaidi nchini.

Ukiacha mtu mmoja mmoja, miongoni mwa wanufaika ni baadhi ya taasisi kama Jumuiya ya Kuhuisha Tabia za Kiislamu (JAI) inayojishughulisha na kuhudumia wagonjwa katika hospitali za nchi nzima na pia taasisi ya Shura ya Maimamu inayohudumia wafungwa.

NA MWANDISHI WETU

# Rais Mwinyi ataka misikiti kuwa chachu ya suluhu za kijamii



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhaj Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amewahimiza waumini wa dini ya Kiislamu kuitumia vema misikiti kwa ajili ya kujadiliana na kuzipatia ufumbuzi changamoto zilizopo katika jamii.

Alhaj. Dkt. Mwinyi ameyasema hayo, tarehe 24 Aprili 2026, alipojumuika na waumini wa dini ya Kiislamu katika Sala ya Ijumaa iliyoambatana na ufunguzi wa Msikiti Mpya wa Jamaa Nour uliopo Boshowa, Nungwi, Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Ameeleza kuwa zipo changamoto nyingi katika jamii zinazohitaji kupatiwa ufumbuzi, hususan zile wanazokabiliana nazo watu wa makundi maalumu, wakiwemo wajane, wazee wasiojiweza, watoto, watu wenye ulemavu na mayatima.

Aidha, Alhaj Dkt. Mwinyi amesema waumini wana wajibu mkubwa wa kuitumia misikiti kusomesha dini, hususan kwa watoto ili waijue vema dini yao, pamoja na kusali kwa bidii na kumcha Mwenyezi Mungu, kwani hiyo ndiyo sababu kuu ya kujengwa misikiti mikubwa na mizuri katika maeneo mbalimbali.

Vilevile, Alhaj Dkt. Mwinyi amewahimiza waumini kuutunza msikiti huo mpya ili ubaki katika haiba na mazingira bora wakati wote, kwa kuweka utaratibu mzuri wa kuchangia, pamoja na kuwatunza maimamu na walimu wa madrasa, na kumshukuru mfadhili wa msikiti huo kwa uamuzi wake.



NA MWANDISHI WETU

# Mwinyi ashauri maboresho ya viza kidijitali kwa wageni



Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, ameishauri Wizara ya Mambo ya Ndani kuimarisha mfumo wa utoaji viza kwa njia ya kidijitali ili huduma hiyo ipatikane haraka kwa wageni wanaoingia nchini.

Dkt. Mwinyi ameyasema hayo Aprili 24, 2026 alipokutana na kufanya mazungumzo na Waziri wa Mambo ya Ndani wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Patrobas Katambi, aliyefika Ikulu Zanzibar kwa ajili ya kujitambulisha.

Dkt. Mwinyi amesema kuwa kwa muda mrefu kumekuwepo na tatizo la upatikanaji wa viza kupitia mfumo wa mtandao (online), jambo linalolalamikiwa na watalii wengi wanaoingia nchini na hivyo kutumia muda mrefu kupata huduma hiyo katika viwanja vya ndege.

Amefahamisha kuwa hatua hiyo itaongeza ufanisi na kudhibiti upotevu wa fedha unaotokana na matumizi ya fedha taslimu. Amesema kuwepo kwa mfumo wa kidijitali ni suala la lazima katika utoaji wa viza, na kuitaka wizara kuchukua hatua za haraka kuondoa tatizo hilo.

Aidha, Dkt. Mwinyi ametaka kuwepo kwa uwajibikaji katika viwanja vya ndege, pamoja na kuimarishwa kwa utoaji wa huduma kwa haraka kwa kuhakikisha kuwepo kwa nguvu kazi ya kutosha muda wote na uwajibikaji wenye ufanisi zaidi.

Sambamba na hilo, Dkt. Mwinyi ametoa wito kwa jeshi la polisi kuimarisha usalama katika maeneo ya utalii ili kudhibiti matukio ya uhalifu, pamoja na kuongeza juhudi za kufanya uchunguzi wa haraka pale matukio yanapotokea na kuweka utaratibu mzuri wa utoaji wa taarifa kwa umma. Akizungumzia suala la usalama barabarani, amesema juhudi za ziada zinahitajika kuimarisha utekelezaji wa sheria za usalama barabarani kutokana na kutofuatwa kikamilifu kwa sheria hizo, hali inayochangia ongezeko la ajali za barabarani.

Pia amesisitiza kuimarishwa kwa juhudi za kupambana na udhalilishaji wa kijinsia, tatizo aliloeleza kuwa ni kubwa hapa nchini.

Nae Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Patrobas Katambi, amemuhakikishia Dkt. Mwinyi kuwa wizara hiyo itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa utii na uaminifu, kwa kuzingatia Katiba, sheria na sera za nchi, na kuahidi kuyafanyia kazi maelekezo yote yaliyotolewa.

NA MWANDISHI WETU

# Serikali yaja na mwarobaini kudhibiti unywaji wa pombe




Bohari ya Dawa nchini (MSD) imesema iko mbioni kuanza kuingiza nchini dawa maalumu ya kusaidia kuacha pombe aina ya Naltrexone, ambayo itasambazwa katika hospitali za umma.

Baada ya dawa hizo kupatikana, MSD itatangaza rasmi vituo vya afya vitakavyokuwa vinazisambaza ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma kwa urahisi zaidi. Hatua hiyo imepokelewa kwa matumaini makubwa, hasa ikizingatiwa kuwa uraibu wa pombe una athari kubwa kwa afya, uchumi wa familia na jamii kwa ujumla.

Meneja wa MSD Kanda ya Dodoma, Mwanashehe Jumaa ameeleza hayo Aprili 24, 2026 wakati wa kikao kazi na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari nchini, kilicholenga kujadili maboresho na utekelezaji wa majukumu ya Bohari ya Dawa (MSD).

Amesema dawa hiyo inalenga kusaidia kundi la watu wenye changamoto ya uraibu wa pombe, ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakikosa huduma hiyo katika hospitali za serikali.

"Tumeipata dawa hii kwa gharama nafuu na itasambazwa katika hospitali mbalimbali. Hapo awali ilikuwa vigumu kwa wagonjwa kuandikiwa dawa hizi kutokana na upatikanaji wake kuwa mdogo, lakini sasa hali itabadilika," alisema Mwanashehe.

Amesema MSD imefikia uamuzi huo kwa kushirikiana na Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe, baada ya kufanya tathmini ya mahitaji ya dawa za afya ya akili nchini na kubaini upungufu mkubwa wa dawa zinazosaidia kudhibiti uraibu wa pombe.

Kwa mujibu wa Mwanashehe, dawa hizo tayari zimeagizwa na zitaanza kutumika katika Hospitali ya Mirembe kabla ya kusambazwa katika vituo vingine vya afya nchini. Ameongeza kuwa hatua hiyo itapunguza gharama kwa wananchi, kwani awali dawa hizo zilikuwa zinapatikana zaidi katika hospitali binafsi na maduka ya dawa kwa bei ya juu.

## Takwimu zinasemaje

Takwimu kutoka Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe zinaonesha kuwa kati ya wagonjwa wanaopokea huduma za afya ya akili, takriban asilimia 30 hadi 40 wanahusishwa moja kwa moja na matumizi ya pombe kupita kiasi.

Aidha, hospitali hiyo inapokea mamia ya wagonjwa wapya kila mwaka wenye matatizo ya uraibu wa pombe, hali inayoongeza mzigo kwa mfumo wa afya.

Tafiti zinaonesha kuwa, takribani asilimia 6.8 ya Watanzania wana tatizo la uraibu wa pombe. Kwa wanaume, kiwango ni kikubwa zaidi ya asilimia 11.5 ukilinganisha na wanawake asilimia 2.2.

Katika baadhi ya hospitali kama KCMC, takriban asilimia 30 ya wagonjwa wa akili wanakuwa wameathiriwa na pombe wanapofikishwa hospitalini.

Katika ngazi ya kitaifa, tafiti mbalimbali zinaonesha kuwa matumizi ya pombe nchini yako juu ukilinganisha na wastani wa Afrika Mashariki.

Tafiti za shirika la Afya Duniani (WHO) zinaonesha kuwa wastani wa matumizi ya pombe kwa mtu mzima nchini unakadiriwa kufikia zaidi ya lita 9 kwa mwaka, kiwango kinachochangia ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza, ajali za barabarani na matatizo ya kijamii.

ذُوالقِعدة

**HABARI**
**MASHARIKI YA KATI**

MAHMOUD NYAMGUMA




# Mahujaji waanza safari kwa imani inayoshinda hofu ya vita

Mahujaji kutoka maeneo mbalimbali duniani wameanza safari na wengine washatua nchi Saudi Arabia kutekeleza nguzo ya tano ya Uislamu- Hijja inayotarajiwa kuanza Mei 24 hadi 29 mwaka huu, huku imani yao ikitajwa kuwa kubwa kuliko hofu ya mivutano ya kivita inayoendelea Mashariki ya Kati.

Takribani mahujaji milioni mbili wanatarajiwa kuhudhuria ibada hiyo takatifu jijini Makkah, licha ya changamoto za ongezeko la gharama, wasiwasi wa safari na usalama.

Licha ya kumbukumbu za ajali zilizowahi kutokea, ikiwemo msongamano wa mwaka 2015 uliosababisha vifo vya zaidi ya watu 2,300, licha ya hali ya kudorora kwa usalama, Waumini wengi wanaonesha uthabiti wa kiimani wakielewa kuwa hiyo ni nguzo muhimu ya Uislamu inayopaswa kutekelezwa.

Wachambuzi wa masuala ya Kiislamu wanaeleza kuwa hata katika vipindi vya vita kama vile mgogoro wa Iran na Iraq, Hija iliendelea kufanyika kwa amani.

Miongoni mwa mataifa ambayo mahujaji wake wameanza kuwasili katika mji mtakatifu wa Makkah ni Indonesia na Malaysia huku serikali zao zikichukua hatua kali za usalama kutokana na mvutano unaoendelea Mashariki ya Kati. Kundi la kwanza la mahujaji wa Indonesia limewasili likiwa sehemu ya zaidi ya mahujaji 204,000 wanaotarajiwa kushiriki ibada ya Hajj mwaka huu. Kwa upande wa Malaysia, kundi la kwanza la mahujaji tayari limewasili Makkah, likianza rasmi safari ya ibada hiyo muhimu ya Kiislamu. Serikali ya nchi hiyo imehakikisha kuwa huduma zote muhimu zinapatikana ili kuhakikisha mahujaji wanatekeleza ibada kwa utulivu na usalama.

Asia ina zaidi ya Waislamu bilioni 1.3, sawa na karibu theluthi mbili ya Waislamu wote duniani, jambo linaloifanya kuwa chanzo kikuu cha mahujaji. Ukiacha Indonesia, baadhi ya nchi nyingine za Asia zinazopeleka mahujaji wengi ni Pakistan 180,000; India 175,025, Bangladesh 78,000 na Malaysia 31,000.

Hijja ni chanzo kikubwa cha mapato kwa taifa la Saudi Arabia ambapo ripoti za uchumi zikionesha kuwa Hijja na Umrah huchangia zaidi ya dola bilioni 12 kila mwaka katika uchumi wa Saudi Arabia, ingawa kwa mwaka huu ibada hiyo inafanyika katika mazingira yenye tahadhari kubwa ya kiusalama kwa nchi mwenyeji Saudi Arabia na hata nchi zinazopeleka mahujaji.

UKHTI FATIMA SS

# Saudi yazindua mfumo wa kidijitali kufuatilia msongamano Msikiti Mkuu

Mamlaka ya Usimamizi wa Msikiti Mkuu wa Makkah imezindua huduma mpya ya kidijitali inayowawezesha Waumini kufuatilia kwa wakati halisi kiwango cha msongamano katika maeneo ya Twawafu na Sa'i ndani ya Msikiti Mtakatifu.

Huduma hiyo inatumia alama za rangi kuonesha hali ya msongamano—ikiwa ni mdogo, wa kati au mkubwa—na hivyo kuwasaidia Waumini kuchagua muda na njia sahihi za kutekeleza ibada zao kwa utulivu zaidi.

Kwa mujibu wa mamlaka hiyo, mfumo huo umeundwa kusaidia kusambaza vizuri mtiririko wa watu, kupunguza msongamano na muda wa kusubiri, pamoja na kuongeza ufanisi wa usimamizi wa umati hasa katika vipindi vya msimu wa Umrah vinavyojumuisha idadi kubwa ya mahujaji.

Hatua hii ni sehemu ya juhudi pana za kutumia teknolojia za kisasa na data za moja kwa moja kuboresha huduma kwa wageni wa Nyumba Tukufu ya Allah na kuhakikisha usalama na urahisi wa ibada.

Huduma hiyo tayari inapatikana kupitia jukwaa rasmi la kidijitali la mamlaka husika, na inatarajiwa kuwa na mchango mkubwa katika kuboresha uzoefu wa waumini wanaotekeleza ibada za Umrah.




## Saudi yakaza masharti ya Hajj 2026, vibali vyapewa kipaumbele

Saudi Arabia imetangaza masharti mapya na makali ya kuingia nchini humo kuelekea ibada ya Hajj mwaka 2026, ikisisitiza kuwa ni wale tu wenye vibali rasmi vya Hajj watakaoruhusiwa kuingia Makkah katika kipindi hicho.

Kwa mujibu wa mamlaka za Saudi, visa za kutembelea (visit visa) hazitaruhusiwa tena kutumika kwa ajili ya kutekeleza ibada ya Hajj. Waumini wote wanatakiwa kuwa na visa maalum ya Hajj pamoja na kibali kinachotolewa kupitia njia rasmi zilizoidhinishwa.

Hatua hiyo inalenga kupunguza msongamano mkubwa na kuimarisha usalama wakati wa ibada hiyo inayokusanya mamilioni ya watu kutoka duniani kote. Mamlaka zimeonya kuwa yeyote atakayekiuka masharti hayo atakabiliwa na adhabu kali, ikiwemo faini na uwezekano wa kupigwa marufuku kuingia nchini humo siku zijazo.

Aidha, vibali vya Umrah vitasitishwa kwa muda wakati wa Hajj ili kutoa nafasi kwa mahujaji na kurahisisha maandalizi ya huduma muhimu. Serikali ya Saudi imesisitiza kuwa waumini wanapaswa kufuata taratibu rasmi ili kuhakikisha ibada inafanyika kwa utulivu, usalama na ufanisi zaidi.

# Waumini 70,000 waswali Ijumaa Al-Aqsa, licha ya vikwazo

Takribani waumini 70,000 waliswali Swala ya Ijumaa katika Msikiti wa Al-Aqsa, licha ya vikwazo vikali vilivyowekwa na vikosi vya Israel katika eneo la Mji wa Kale wa Jerusalem na milango yake.

Mashuhuda wanasema vikosi hivyo viliongeza ulinzi na kudhibiti kwa ukali harakati za waumini wanaoingia katika eneo la msikiti huo, hali iliyosababisha changamoto kwa baadhi ya waabudu kufika kwa wakati.

Katika tukio jingine, vikosi hivyo vilimtoa nje ya eneo hilo mwanaharakati Mohammad Abu Hamzah pamoja na Nafisa Khweis mwenye umri wa miaka 70 na Nizam Abu Ramuz, na kuwazuia kuswali ndani ya msikiti huo.

Wakati huo huo, maafisa wa manispaa walitoza faini kwa Waumini waliokuwa wameegesha pikipiki karibu na lango la Bab al-Sahira, hatua iliyopingwa na wengi. Pamoja na vikwazo hivyo, idadi kubwa ya Waislamu waliendelea kujitokeza kwa ibada, wakionesha mshikamano na umuhimu wa Al-Aqsa kwa Waislamu duniani.




ذُو الْقِعْدَة



MAHMOUD NYAMGUMA

# Nchi 8 zenye Waislamu wengi zalaani uvamizi wa Al-Quds



Mawaziri wa mambo ya nje kutoka nchi nane zenye Waislamu wengi wamelaani vikali Israel kwa kile walichokitaja kuwa ukiukwaji wa mara kwa mara wa hadhi ya kihistoria na kisheria ya maeneo matakatifu ya Kiislamu na Kikristo mjini Jerusalem.

Katika taarifa ya pamoja iliyotolewa Aprili 24, Saudi Arabia, Jordan, Falme za Kiarabu (UAE), Qatar, Indonesia, Pakistan, Misri na Uturuki walieleza wasiwasi wao kuhusu uvamizi unaoendelea katika eneo la Msikiti wa Al-Aqsa, ukifanywa na walowezi wa Kiyahudi na baadhi ya viongozi wenye misimamo mikali chini ya ulinzi wa polisi wa Israel.

Taarifa hiyo ilisisitiza kuwa vitendo hivyo ni ukiukwaji wa wazi wa sheria za kimataifa, haki za kibinadamu, hadhi ya maeneo hayo na pia ni uchokozi unaowaudhi Waislamu duniani kote. Mawaziri hao walikataa jaribio lolote la kubadilisha hali iliyopo kihistoria katika mji wa Jerusalem na maeneo yake matakatifu.

Katika taarifa yao, mataifa hayo yamesema matukio ya hivi karibuni, yakiwemo kuingizwa kwa bendera ya Israel ndani ya viunga vya Msikiti wa Al-Aqsa, ni uchochezi unaogusa hisia za Waislamu duniani. Aidha, walisisitiza kuwa eneo lote la Al-Aqsa ni mahali pa ibada kwa Waislamu pekee, likisimamiwa na Waqf ya Jordan. Pia walilaani ujenzi haramu wa makazi mapya ya walowezi na vitendo vya ukatili dhidi ya Wapalestina.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, uvamizi huo umeongezeka tangu kuanza kwa vita vya Gaza Oktoba 2023, huku walowezi na baadhi ya viongozi wenye misimamo mikali wakiripotiwa kuingia katika eneo la Al-Aqsa chini ya ulinzi wa polisi.

Takwimu kutoka taasisi za Kipalestina zinaonesha kuwa zaidi ya Wapalestina 23,000 wamekamatwa katika Ukingo wa Magharibi na Mashariki mwa Al-Quds tangu kipindi hicho, hali inayoongeza mvutano na kuhatarisha juhudi za amani. Aidha, mawaziri hao wamekosoa vikali uamuzi wa Israel kuidhinisha zaidi ya makazi mapya 30 katika Ukingo wa Magharibi mapema mwezi Aprili 2026, wakieleza kuwa hatua hiyo inahujumu uwezekano wa kuundwa kwa dola huru ya Palestina. Ripoti mbalimbali za kimataifa, ikiwemo za mashirika ya haki za binadamu, zimekuwa zikionya kuwa ongezeko la makazi hayo na vitendo vya ukatili dhidi ya raia vinaongeza hatari ya kuzorota kwa usalama wa kikanda.

Wachambuzi wa siasa za kimataifa wanaeleza kuwa kuendelea kwa hali hii kunaweza kudhoofisha juhudi za kidiplomasia na kuongeza hatari ya mgogoro mpana zaidi katika eneo hilo nyeti duniani. Mawaziri hao waliitaka jumuiya ya kimataifa kuchukua hatua za haraka kusitisha ukiukwaji huo na kusukuma mbele suluhisho la mataifa mawili kama msingi wa amani ya kudumu.

MAHMOUD NYAMGUMA

# Mataifa ya Kiislamu yakemea uteuzi wa balozi wa Israel Somaliland



Mataifa 16 ya Kiarabu na Kiislamu yamelaani vikali uamuzi wa Israel kuteua balozi wake katika eneo la Somaliland, yakitaja hatua hiyo kuwa ukiukwaji wa wazi wa mamlaka, umoja na mipaka ya Somalia.

Katika taarifa ya pamoja iliyotolewa mwishoni mwa wiki, mawaziri wa mambo ya nje kutoka nchi zikiwemo Saudi Arabia, Misri, Pakistan na Uturuki wamesisitiza kuwa hatua hiyo inakinzana na sheria za kimataifa na Mkataba wa Umoja wa Mataifa.

Taarifa hiyo imeonya kuwa uteuzi huo unaweza kuweka mfano hatari unaoweza kudhoofisha utulivu wa eneo hilo la Pembe ya Afrika linalokabiliwa na changamoto za kiusalama. Kwa mujibu wa takwimu za taasisi za kimataifa, eneo hilo lina zaidi ya watu milioni 150 wanaotegemea utulivu wa kisiasa na usalama kwa maendeleo ya kiuchumi, huku migogoro ikiathiri ukuaji wa uchumi kwa wastani wa asilimia 1–2 kila mwaka.

Nchi hizo zimeeleza kuwa mshikamano wa kimataifa unapaswa kuheshimu uhuru wa mataifa yaliyo wanachama wa Umoja wa Afrika, hasa Somalia ambayo bado inakabiliwa na vitisho vya kiusalama ikiwemo makundi yenye misimamo mikali.

Wachambuzi wa siasa za kimataifa wanaona kuwa msimamo huo wa pamoja wa mataifa ya Kiislamu unaashiria kuimarika kwa diplomasia ya pamoja katika kulinda maslahi ya kikanda. Wanasema kuwa ikiwa hatua kama hizi hazitadhibitiwa, zinaweza kuongeza migogoro ya kidiplomasia na kuathiri juhudi za kulinda amani na usalama katika ukanda mzima wa Afrika Mashariki na Pembe ya Afrika.



UKHTI FATIMA SS




# AlHuda CIBE yashirikiana na AIID kuendeleza fedha za Kiislamu Afrika

Taasisi ya Kimataifa ya Ushauri na Mafunzo katika Sekta ya Fedha za Kiislamu, AlHuda Centre of Islamic Banking and Economics (CIBE), imeingia makubaliano ya kimkakati na kampuni ya Agency for Inclusive Innovations Development (AIID) Limited ili kuharakisha upanuzi wa huduma za kifedha zinazozingatia Sharia barani Afrika.

Ushirikiano huo, uliotangazwa Aprili 21, 2026 mjini Dubai, unalenga kukuza ujumuishaji wa kifedha, hususan katika masoko yanayoibukia kama Kenya. Taasisi hizo mbili zitatoa huduma za ushauri, kufanya tafiti za upembuzi yakinifu, kuendesha mafunzo ya kitaalamu na kusaidia ubunifu wa bidhaa za kifedha zinazokidhi mahitaji ya ndani.

Mtendaji Mkuu wa AlHuda CIBE, Muhammad Zubair Mughal, amesema ushirikiano huo utaimarisha uwezo wa ndani na kuwezesha maendeleo ya suluhisho za kifedha zinazozingatia maadili ya Kiislamu.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa AIID, Dk. Hassan Bashir, amesema hatua hiyo ni muhimu katika kuimarisha mifumo jumuishi ya kifedha barani Afrika.

Hatua za awali zitahusisha mafunzo, tafiti za soko na miradi ya majaribio ili kupanua upatikanaji wa huduma za fedha za Kiislamu.



## Senegal yazindua mfuko wa Kiislamu kuwezesha wajasiriamali 300,000 wadogo

**Serikali ya Senegal imezindua Mfuko wa Maendeleo ya Mikopo Midogo ya Kiislamu (FDMI) wenye lengo la kuimarisha upatikanaji wa mitaji kwa wajasiriamali wadogo na wa kati, hasa katika maeneo ya vijijini. Mfuko huo unatarajiwa kukusanya faranga za CFA bilioni 200 (takribani dola milioni 357.6) ndani ya miaka mitano ili kufadhili miradi 300,000.**

**Akizungumza wakati wa uzinduzi huo Aprili 21, Waziri wa Mikopo Midogo, Alioune Dione, alisema mfuko huo utatumia rasilimali zinazozingatia misingi ya Sharia, ikiwemo mfumo wa kugawana faida na hasara, ili kusaidia biashara ndogo, vijana na wanawake.**

**Mkuu wa mfuko huo, Abdou Diaw, alieleza kuwa FDMI pia utasaidia kupanga na kuelekeza vyema mtiririko wa fedha katika sekta hiyo.**

**Mfuko huo unachukua nafasi ya programu ya "Promise" iliyoanzishwa mwaka 2018 kwa ushirikiano na Benki ya Maendeleo ya Kiislamu, na unalenga kuwa na mfumo imara zaidi wa usimamizi pamoja na upanuzi wa kitaifa.**

**Ingawa asilimia 94 ya wananchi wa Senegal ni Waislamu, huduma za fedha za Kiislamu bado ni ndogo, zikichangia takribani asilimia 8.3 ya mali za benki mwaka 2024. Hatua hii inaonekana kuongeza ujumuishaji wa kifedha nchini humo.**

## IMAN Holding yazindua mpango wa benki ya Kiislamu inayotumia AI

**Kampuni ya IMAN Holding imetangaza mpango mkubwa wa kuendeleza jukwaa la benki ya Kiislamu linalotumia teknolojia ya akili bandia (AI), huku ikilenga kupanua huduma zake kimataifa.**

**IMAN Holding ni kampuni ya teknolojia ya kifedha (fintech) inayojikita katika kuunganisha huduma za kifedha na kanuni za Kiislamu, ikitumia AI kutoa suluhisho za benki zinazobinafsishwa na kuendana na Sharia.**

**Tangazo hilo linaambatana na jitihada za kukusanya dola milioni 100 ili kufadhili maendeleo ya teknolojia, upanuzi wa masoko, na kupata leseni kamili ya benki ya Kiislamu.**

**Kwa mujibu wa mwanzilishi na Mkurugenzi Mkuu, Rustam Rahmatov, changamoto ya benki za sasa si upatikanaji wake bali namna zilivyoundwa, akisema mifumo mingi "haikuundwa kuelewa watu." Jukwaa hilo linatumia AI kuchambua mienendo ya kifedha ya watumiaji, kufanya maamuzi ya kifedha kwa wakati halisi, na kutoa mapendekezo yanayozingatia muktadha wa mtumiaji—yote ndani ya mfumo unaozingatia kanuni za Sharia.**

**Kampuni hiyo tayari ina zaidi ya watumiaji milioni moja na inasimamia zaidi ya dola milioni 100 katika mali, ikilenga kufikia zaidi ya dola milioni 250 ifikapo mwisho wa 2026.**

**IMAN pia inalenga kupanua shughuli zake katika eneo la Ghuba (GCC), ambapo kuna mahitaji makubwa ya huduma za kifedha za Kiislamu pamoja na mazingira rafiki ya kisheria.**

**Hatua hii inaashiria mwelekeo mpya katika sekta ya fedha: kuunganisha teknolojia ya kisasa na maadili ya Kiislamu ili kujenga mfumo wa benki unaoelewa zaidi tabia za watumiaji.**

ذُوالقِعدة

KUTOKA KWA MAJIRANI

NA MUGINI SINGIRA

# Uganda yakumbuka kifo cha kiongozi maarufu wa Kiislamu Prince Badru


Uganda leo inakumbuka kifo cha mmoja wa viongozi wake mashuhuri wa kidini na kisiasa, Prince Badru Kakungulu, aliyefariki Aprili 24, 1991, akihitimisha enzi muhimu katika historia ya Waislamu wa nchi hiyo.

Kakungulu, aliyezaliwa mwaka 1907, alikuwa wa ukoo wa kifalme wa Buganda na mtoto wa Prince Nuhu Mbogo, aliyekuwa kiongozi wa Waislamu baada ya vita vya kidini vya miaka ya 1880. Baada ya kifo cha baba yake mwaka 1921, Kakungulu alirithi uongozi huo akiwa na umri wa miaka 14.

Chini ya uongozi wake, Kibuli Hill iligeuka kuwa kitovu cha Uislamu nchini Uganda. Alichangia kuanzishwa kwa taasisi muhimu kama Msikiti wa Kibuli, Shule ya Sekondari Kibuli na Hospitali ya Kibuli. Pia alikuwa mtetezi wa elimu, akishiriki kuanzisha Chama cha Elimu ya Kiislamu Uganda mwaka 1947.

Kisiasa, alikuwa miongoni mwa waanzilishi wa chama cha Kabaka Yekka na alichangia muungano uliosaidia Uganda kupata uhuru mwaka 1962. Hata hivyo, alikumbwa na changamoto mwaka 1966 alipokamatwa wakati wa mgogoro wa kisiasa uliovunja falme za jadi.

Anakumbukwa kama kiongozi wa msimamo wa kati na mleta mageuzi, aliyekuwa na mchango mkubwa katika historia ya Uganda. Baadhi ya majina maarufu aliyopewa ni 'Kabaka wa Waislamu', 'Babu wa Waislamu wa Uganda', 'Baba wa Elimu ya Waislamu Uganda.'



UKHTI FATIMA SS

# Benki ya kwanza ya Kiislamu Kenya yapata mwekezaji Dubai



Benki ya Gulf African Bank ya Kenya imepata mwekezaji mpya kutoka Dubai baada ya kampuni ya Soren Investment Company kushirikiana na Auron Holdings ya Nairobi kununua kwa pamoja asilimia 57.72 ya hisa za benki hiyo.

Katika mpango huo, Soren Investment Company imenunua asilimia 42.78 ya hisa kutoka Al Salam Bank na Istithmar World Limited, huku Auron Holdings ikichukua asilimia 14.94 kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC). Ununuzi huo umeondoa baadhi ya wawekezaji wakongwe waliokuwa na ushawishi mkubwa katika benki hiyo.

Taarifa rasmi ya benki imethibitisha kuwa taratibu zote za kisheria na udhibiti zimekamilika, na mamlaka husika nchini Kenya zimeridhia mabadiliko hayo ya umiliki.

Soren Investment Company ni kampuni ya uwekezaji iliyosajiliwa katika Kituo cha Fedha cha Kimataifa cha Dubai (DIFC) mwaka 2019, ikiwa na mkakati wa kupanua uwekezaji wake katika sekta ya benki za Kiislamu barani Afrika. Tayari ina umiliki mkubwa katika taasisi za kifedha nchini Sudan na Tanzania. Kwa upande wake, Auron Holdings ni kampuni ya ndani inayomilikiwa na wawekezaji wa Kenya, ikilenga kupanua uwekezaji wake kwa muda mrefu.

Hatua hii inaashiria juhudi za kujenga mtandao mpana wa benki za Kiislamu Afrika Mashariki, huku Gulf African Bank ikiendelea kuimarika kifedha baada ya kurekodi faida ya shilingi bilioni 1.35 mwaka 2024.

# Wanaharakati Kenya hoi baada ya utoaji mimba bila sababu kuharamishwa

Katika mgeuko mkubwa wa kisheria, Mahakama ya Rufaa nchini Kenya imebatilisha uamuzi wa Mahakama Kuu uliokuwa umetambua utoaji mimba kama haki ya msingi ya kikatiba, na hivyo kurejesha vikwazo vikali vinavyodhibiti huduma hiyo.

Uamuzi huo uliotolewa Ijumaa unahitimisha hatua muhimu katika mzozo wa muda mrefu uliogawanya maoni ya umma, huku ukitarajiwa kupelekwa Mahakama ya Juu kwa uamuzi wa mwisho.

Chanzo cha kesi hiyo ni tukio la mwaka 2022 lililomhusisha msichana aliyepata matatizo ya ujauzito na kupatiwa huduma ya dharura hospitalini baada ya kupoteza mimba. Mahakama Kuu wakati huo iliamua kuwa upatikanaji wa huduma za utoaji mimba ni haki ya kikatiba, na kuharamisha kukamatwa au kushtakiwa kwa wagonjwa na wahudumu wa afya katika mazingira hayo.

Hata hivyo, Mahakama ya Rufaa sasa imesisitiza kuwa Katiba inalinda haki ya uhai wa mtoto, na kwamba utoaji mimba unaruhusiwa tu katika hali maalum, ikiwemo pale maisha ya mama yako hatarini.

Makundi ya haki za binadamu yameelezea uamuzi huo kama hatua ya kurudisha nyuma juhudi za kulinda afya ya wanawake, huku upande wa mashirika ya kidini ukiusifu kama kurejesha mizani ya kikatiba.

Kisheria, mtu anayehusika na utoaji mimba anaweza kuhukumiwa kifungo cha hadi miaka 14 jela, jambo linaloonesha uzito wa mjadala huu nchini Kenya..

Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania

Mhariri
+255 789 201383

# Tupeleke elimu ya zaka misikitini

Zaka ni ibada yenye athari kubwa si tu kwa mtoaji, bali pia kwa jamii nzima ya Kiislamu. Hata hivyo, pamoja na umuhimu wake, bado kuna ombwe la uelewa sahihi kuhusu zaka miongoni mwa Waislamu.

Hali hii inaonesha haja ya kueneza elimu ya zaka kupitia majukwaa muhimu ya dini, hususan misikiti. Allah Mtukufu amewajibisha zaka sambamba na sala tano, aliposema: "Na simamisheni sala na toeni zaka..." [Qur'an, 2:43].

Aya inaonesha umuhimu na uzito wa nguzo ya zaka katika Uislamu. Pamoja na hilo, utekelezaji sahihi wa ibada hii hauwezi kufikiwa bila elimu ya kutosha kuhusu viwango (nisab), masharti, aina ya mali zinazotolewa zaka pamoja na walengwa wake.

Misikiti kama nyumba za ibada na malezi ya kiroho kwa Waislamu inapaswa kubeba jukumu la kufikisha mafundisho ya dini kwa umma kupitia khutba, darsa na mawaidha.

Hivyo basi, ni wajibu wa Masheikh, maimamu na wanazuoni kutumia majukwaa haya kuwaelimisha waumini kuhusu ibada ya zaka kwa undani na kwa ufasaha. Ni kupitia elimu sahihi ndipo Waislamu wataweza kutekeleza kikamilifu ibada hii muhimu.

Misikiti inaweza kuwa kiungo muhimu katika kusimamia ukusanyaji na ugawaji wa zaka kwa uwazi na ufanisi. Hata hivyo, mafanikio ya jukumu hili yanategemea kwa kiasi kikubwa uelewa wa waumini kuhusu umuhimu wa kushirikiana na taasisi za dini katika kusimamia ibada hii.

Elimu ya zaka itasaidia kujenga mfumo madhubuti wa kuwasaidia wahitaji, kuwaongoza Waislamu wanaotoa zaka bila kufuata utaratibu sahihi wa kisharia pamoja na kuwahamasisha wale wasiotoa kabisa. Vilevile, itachangia kujenga imani na uwajibikaji ndani ya jamii ya Kiislamu. Waislamu wanapofahamu kuwa zaka si hiari bali ni wajibu wa kisharia hupata motisha ya kuitoa kwa ikhlas na kwa wakati.

## Baadhi ya faida za kutoa zaka

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) ameeleza umuhimu wa zaka na athari zake kwa jamii alipomwambia Muadh bin Jabal: "Wajulishe (watu wa Yemen) kuwa Allah amewafaradhishia sadaka (zaka) inayochukuliwa kutoka kwa matajiri wao na kurejeshwa kwa masikini wao." [Bukhari na Muslim].

Hadith hii inaonesha dhima ya zaka kama chombo cha kupunguza pengo kati ya matajiri na masikini. Hata hivyo, inastaajabisha kuona kwamba wapo Waislamu wenye uwezo wa kutoa zaka lakini hawafanyi hivyo. Aidha, kuna wale wanaotoa lakini hawazingatii makundi yaliyotajwa na Allah ndani ya Qur'an, wakiwamo mafukara na masikini.


Kutoa zaka, pia huongeza baraka katika mali ya muumini na kuleta mafanikio ya kweli, huimarisha mshikamano wa kijamii na kupunguza umasikini, chuki za kitabaka pamoja na uhalifu unaotokana na hali ngumu ya maisha.

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Mali haipungui kwa kutolewa sadaka." [Muslim]. Zaidi ya hayo, zaka huchochea hisia za undugu, umoja na mshikamano, na huondoa hisia za kutengwa au upweke kwa masikini, hivyo kuimarisha usawa wa kijamii na kupunguza migogoro inayoweza kujitokeza kutokana na umasikini.



# HABARI ZA MASHARIKI YA KATI

UKHTI FATIMA SS




Strait of Hormuz ni njia nyembamba ambayo karibu asilimia 20 ya mafuta na gesi ya dunia hupitia kila siku. Kwa maneno mengine, sehemu hii ndogo kati ya Iran na Oman ndiyo inabeba sehemu kubwa ya mfumo wa nishati wa dunia. Ikivurugika, athari zake huenea haraka kutoka masoko ya mafuta hadi bei za chakula na bidhaa za viwandani.

Umuhimu wake wa kisasa una mizizi ya kihistoria. Ingawa eneo hili limekuwa la kimkakati kwa karne nyingi—hata mataifa ya Ulaya yalilipigania wakati wa enzi za meli za kale—uzito wake uliongezeka sana baada ya kugunduliwa kwa mafuta katika Ghuba ya Uajemi katika karne ya 20.

Kuanzia miaka ya 1930, ugunduzi mkubwa wa mafuta Bahrain na Saudi Arabia ulifanya Hormuz kuwa njia kuu ya kusafirisha rasilimali hizi kwenda duniani. Kufikia miaka ya 1950, mafuta yaliyopita hapa yalikuwa yakichochea ujenzi wa upya wa uchumi wa dunia baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia.

Leo, nafasi yake katika uchumi wa dunia ni muhimu sana. Takriban mapipa milioni 20 ya mafuta na bidhaa zake, zinazofikia thamani ya dola bilioni 600 kwa mwaka hupita hapa kila siku. Aidha, zaidi ya mita za ujazo bilioni 112 za gesi asilia iliyoyeyushwa (LNG)—karibu asilimia 20 ya biashara ya dunia—hupitia hapa. Qatar, mmoja wa wauzaji wakubwa wa LNG, inategemea kabisa njia hii, jambo linaloonyesha kuwa hakuna mbadala rahisi wa usafirishaji wa gesi.

Lakini athari zake hazikomei kwenye nishati. Kwa mujibu wa uchambuzi wa Al Jazeera Centre for Studies, Hormuz inaunganisha pia masoko ya viwanda na chakula. Eneo la Ghuba huzalisha karibu asilimia 44 ya sulphur ya dunia—kiungo muhimu katika mbolea na uzalishaji wa metali kama shaba na nikeli.

Zaidi ya hapo, karibu theluthi moja ya biashara ya mbolea duniani hupitia njia hii. Hii ina maana kwamba kuvurugika kwa Hormuz kunaweza kuathiri moja kwa moja uzalishaji wa chakula na hata sekta ya teknolojia kama utengenezaji wa semiconductor.

Hali ya sasa ya kisiasa imeonyesha wazi udhaifu wa utegemezi huu. Kufuatia mvutano wa kijeshi mwaka 2026, kiwango cha meli zinazopita kilishuka kwa 95% , huku bei ya mafuta ikipanda na masoko ya gesi Ulaya yakiongezeka kwa zaidi ya asilimia 60 ndani ya siku chache. Nchi za Asia, ambazo hupokea hadi asilimia 80–89 ya mafuta yanayopita hapa, zilihisi athari kubwa zaidi. Hata maisha ya kila siku yalibadilika—kupungua kwa umeme, kufungwa kwa taasisi, na hatua za dharura za matumizi ya nishati katika baadhi ya nchi. Hata hivyo, hoja muhimu inayojitokeza ni mipaka ya nguvu za kijeshi. Ingawa taifa linaweza kutishia kufunga au kufungua njia hii, kufanya hivyo kwa muda mrefu si rahisi. Uchambuzi unaonyesha kuwa operesheni ya kijeshi ya kurejesha usafiri ingekuwa ghali, ya muda mrefu, na yenye hatari kubwa kutokana na makombora, mabomu ya baharini na ndege zisizo na rubani. Zaidi ya hayo, jiografia ya eneo—ikiwa nyembamba na karibu na pwani ya Iran—inaipa nchi hiyo faida ya kimkakati ambayo si rahisi kuondoa. Kwa mtazamo wa siasa za dunia, Hormuz imekuwa chombo cha ushawishi. Mataifa yanayotegemea nishati kutoka Ghuba yanahitaji njia hii ibaki wazi, wakati Iran inaweza kutumia udhibiti wake kama njia ya kujadiliana. Hii inaunda hali ya "mutual vulnerability"—yaani, kila upande unategemea mwingine kwa kiwango fulani.

Pamoja na juhudi za kutafuta njia mbadala—kama mabomba ya mafuta yanayopita nje ya Hormuz—uchambuzi wa Jukwaa la Uchumi la Dunia (WEF) unaonyesha kuwa hakuna suluhisho rahisi, hasa kwa bidhaa kama gesi, mbolea na sulphur ambazo zinahitaji miundombinu mipya ya gharama kubwa. Hivyo, dunia itaendelea kuitegemea njia hii kwa muda mrefu ujao.

ذو القعدة

## NASAHA ZA WIKI

0787 503 085

NA YUSUFU AMINI



# Athari ya miezi Mitakatifu katika kudumisha ibada



Allah Mtukufu ameitaja miezi Minne Mitakatifu kuwa ni nyakati zenye thamani na heshima ya pekee kwa waumini. Anasema: "Hakika idadi ya miezi mbele ya Allah ni (miezi) kumi na miwili katika hukumu ya makadirio ya Allah, tangu siku aliyoumba mbingu na ardhi. Kati ya hiyo, ipo minne mitakatifu. Hiyo ndiyo dini ya sawa, kwa hiyo msizidhulumu nafsi zenu ndani yake (miezi hiyo)." [Qur'an, 9:36].

Miezi Mitakatifu iliyokusudiwa hapa ni mwezi huu wa Dhul–Qa'ada (Mfunguo pili), Dhul–Hijja (Mfunguo tatu), Muharram (Mfunguo nne) na mwezi wa Rajab, kama alivyosimulia Sahaba Mtukufu, Abibakr (Allah amridhie) katika hadith isemayo: "Zama zimekamilisha mzunguko wake na imekuwa kama ilivyokuwa siku Allah alipoumba mbingu na ardhi. Mwaka una miezi kumi na miwili na katika hiyo minne ni mitakatifu, mitatu imefuatana – Dhul – Qa'ada, Dhul–Hijja, Muharram na Rajab Mudharr ulio kati ya Jumaada (Aakhir) na Shaaban." [Bukhari na Muslim].

Katika kuifafanua miezi hii minne, wanazuoni wa fani ya historia (Tareikh) wamesema kuwa, Allah ameiteua miezi hii kuwa Mitakatifu na kukataza watu kupigana vita ndani yake kwa sababu maalumu, nayo ni kuwawezesha Waislamu kwenda Makka kufanya ibada ya Hijja na Umra na kurejea nyumbani kwa amani.

Hii inaonesha kuwa miezi hii si tu ya kutekeleza ibada binafsi bali pia kuimarisha maadili ya kijamii kama amani, uvumilivu, na mshikamano miongoni mwa wanajamii. Moja ya sifa kuu za miezi hii ni kwamba, ilikuwa ikiheshimiwa hata kabla ya Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) kupewa Utume.

Katika miezi hii, Waislamu wanahimizwa kuepuka maasi kama shirk, wizi, zinaa, kulewa, kudhulumiana, kugombana, kutukanana, kuvunjiana heshima, kusengenya na kusema uongo. Kiujumla, Waislamu wanatakiwa kuitumia miezi hii katika kujikurubisha zaidi kwa Allah, kutakasa nafsi, kufanya toba ya kweli, na kuongeza juhudi katika ibada.

Pamoja na faida lukuki zinazopatikana ndani ya miezi hii, inasikitisha kuona wengi wetu hatuipi umuhimu kama ilivyo kwa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan, na ndiyo maana tumekuwa tunatumia muda mwingi kushughulikia mambo yasiyo na faida.

Kwa hali hii, si ajabu wapo miongoni mwetu Waislamu ambao hawafahamu umuhimu na fadhila za miezi tuliyonayo. Hivyo, ipo haja kwa viongozi wa dini, hususan maimam wa misikiti, kuwaelimisha waumini juu ya fadhila zake na kuwahamasisha kufanya mambo ya kheri.

### Yaliyohimizwa kufanywa katika Miezi Mitakatifu

Kuna amali nyingi njema ambazo Muislamu anaweza kuzifanya katika miezi hii, lakini jambo la msingi ni kujitahidi kufanya mema kadiri ya uwezo wake. Allah Ta'ala anasema: "Basi mcheni Mwenyezi Mungu kadiri muwezavyo, na sikieni, na tiini, na toeni; itakuwa kheri kwa nafsi zenu. Na mwenye kuepushwa na uchoyo wa nafsi yake, basi hao ndiyo waliofanikiwa." [Qur'an, 64:16].

Kwa msingi huo, Muislamu anapaswa kujibidiisha katika ibada mbalimbali kama kusoma Qur'an, kufunga swaumu za sunna, kuomba msamaha, kutubia madhambi, kumdhukuru Allah kwa wingi, kusaidia wahitaji, kutenda mema kwa majirani na marafiki, pamoja na kupatanisha waliogombana. Aidha, ni vyema kutambua kuwa kila neema aliyopewa mwanadamu ataulizwa Siku ya Kiyama. Hivyo basi, ni wajibu kuitumia vyema fursa ya afya na uhai katika kumtumikia Allah, kwani amali njema katika miezi hii huambatana na ujira mkubwa.

Ingawa kumuasi Allah hakuruhusiwi katika miezi yote kumi na miwili, dhambi zinazofanywa katika miezi Mitakatifu huwa na uzito zaidi.

Imam Qatada anasema: "Dhuluma itakayotendeka katika miezi Mitakatifu ni mbaya na kubwa zaidi kuliko inayotendeka katika miezi mingine. Ingawa dhuluma ni kosa wakati wote, Allah huifanya baadhi ya mambo kuwa mazito zaidi kuliko mengine." [Tafsiri ya Qur'an–Ibn Kathir].

Kwa hiyo, tujihimu kuitukuza miezi hii Mitakatifu na kukithirisha ibada ndani yake kwani ni miezi iliyobarikiwa inayoweza kubadilisha maisha yetu ya kiroho na kijamii. Pia tuepuke mambo yaliyoharamishwa kwa kuzingatia maonyo ya Allah Aliyetukuka: "Enyi mliyoamini, msivunje utukufu wa alama za Allah wala miezi Mitakatifu..." [Qur' an, 5:2].



SHEIKH
Seif Ruga
0712 690 811

# Kuamini qadar kama njia ya kukabili tatizo la kujiua

**Nafsi ya mwanadamu ni mali ya Allah Mtukufu, na uhai ni zawadi aliyompa mwanadamu. Kwa msingi huo, si halali kwa mtu kujiua, kwani kufanya hivyo ni kuingilia jambo asilolimiliki.**
**Allah Mtukufu anasema: "...wala msiziue nafsi zenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye kuwarehemu. Na atakayefanya hivyo kwa ujeuri na dhuluma tutamuingiza Motoni. Na hilo kwa Mwenyezi Mungu ni jepesi mno." [Qur'an, 4:29–30].**

Katika mafundisho ya Uislamu, dhana ya uhuru binafsi haimaanishi kufanya lolote apendalo mtu, bali uhuru huo una mipaka ya utumwa na utii kwa Allah. Hivyo basi, kujiua si suluhisho la matatizo ya maisha, kwa kuwa maisha hayaishii duniani pekee, bali yanaendelea kaburini (Barzakh) na baadaye Akhera.

Uislamu unakataza kujiua kwa njia yoyote ile – iwe kwa kujidhuru, kuharibu kiungo, au kutumia chakula na vinywaji vyenye sumu. Adhabu ya aliyejiua inatekelezwa Akhera, siyo duniani, kwani wanadamu hawawezi kumwadhibu maiti.

Mtume (rehema na amani ya Allah zimshukie) amesema: "Atakayejiua kwa kipande cha chuma atatupwa Motoni akiwa na kipande hicho akijitwanga nacho tumboni milele; na atakayekunywa sumu hadi akafa ataendelea kunywa sumu hiyo ndani ya Moto wa Jahannam milele; na atakayejitupa kutoka mlimani hadi kufa ataendelea kujitupa ndani ya Moto wa Jahannam milele." [Bukhari na Muslim].

Wanazuoni wa sharia ya Kiislamu (Fuqahau) wamefafanua kuwa kujiua ni tendo la mtu kujitoa uhai wake kwa makusudi. Aidha, wamekubaliana kuwa mtu aliyejiua anakuwa ametenda dhambi kubwa kuliko hata yule aliyemuua mtu mwingine, kwa kuwa anakuwa adui wa nafsi yake mwenyewe.

Kwa hali hiyo, mtu aliyejiua anahesabika kuwa ni fasiki na muasi dhidi ya nafsi yake. Baadhi ya wanazuoni wameeleza kuwa mtu aliyejiua hafai kuoshwa wala kuswaliwa sala ya jeneza, wakimlinganisha na muasi aliyepigana dhidi ya Waislamu.

Tafiti mbalimbali zinaonesha kuwa takriban asilimia 35 ya matukio ya kujiua yanahusishwa na magonjwa ya akili na matatizo ya kisaikolojia kama mfadhaiko (depression), ugonjwa wa akili (schizophrenia) na uraibu wa dawa za kulevya.

Vilevile, takriban asilimia 65 ya matukio hayo husababishwa na changamoto za kijamii na kimaisha, ikiwamo malezi, utamaduni wa jamii, migogoro ya kifamilia au kimahusiano, kufeli masomo, maradhi ya mwili, hofu ya fedheha, au kushikamana na fikra zinazoonekana kuhalalisha kujiua.

Kwa mujibu wa mafundisho ya Kiislamu, haipasi Muislamu kutamani kifo kwa sababu ya matatizo ya dunia. Mtume wa Allah amesema: "Mmoja wenu asitamani kifo kwa sababu ya dhiki iliyompata. Na kama hana budi kufanya hivyo, basi na aseme: Ewe Allah, nipe uhai ikiwa uhai ni bora kwangu, na nifishe ikiwa kifo ni bora kwangu." [Bukhari].

Mfano wa subira unaonekana kwa Nabii Ayyub (amani iwe juu yake), ambaye alipoteza mali, watoto na afya, lakini hakukata tamaa. Alimwomba Mola wake akisema: "Hakika mimi yamenipata madhara, na wewe ndiye Mbora zaidi wa kurehemu kuliko wote wanaorehemu." [Qur'an, 21:83]. Hatimaye Allah alimwitikia dua yake na kumrejeshea neema zake, ikiwa ni rehema na funzo kwa waumini.

## Sababu kuu za kujiua

Ukosefu wa imani na mafundisho sahihi ya dini ni miongoni mwa mambo makuu yanayosababisha huzuni, mashaka na taabu zinazowakumba watu wengi siku hizi. Kinyume na mitazamo ya wengi, si umasikini, udhaifu au dhuluma pekee vinavyosababisha hali hiyo.

Mtume amebainisha hilo aliposema: "Yule ambaye hamu yake kubwa ni Akhera, Allah humkusanyia mambo yake, huweka utajiri moyoni mwake, na huiona dunia ni dhalili. Na yule ambaye lengo lake kuu ni dunia, Allah hutawanya mambo yake na huweka hofu ya ufukara mbele ya macho yake..." [Ibn Majah].

Imani thabiti na yakini kwa Allah humfanya mtu kuridhika na maamuzi (qadar) yake, hata pale hali inapokuwa ngumu. Kinyume chake, anayefikia hatua ya kujiua huwa hajaridhika na maamuzi ya Allah.

Uislamu, ambao ni mfumo kamili wa maisha ya mwanadamu unasisitiza umuhimu wa kurejea katika misingi ya imani, subira na matumaini ili kukabiliana na changamoto za maisha bila kufikia hatua ya kujiua.

Takwimu mbalimbali zinaonesha kuwa katika baadhi ya nchi zilizoendelea kiuchumi, viwango vya watu wanaojiua ni vya juu zaidi.

Licha ya kuwepo chakula cha kutosha, makazi bora na anasa nyingi, bado baadhi ya watu huishi katika hali ya huzuni, wasiwasi na msongo wa mawazo.

Watafiti wanaeleza kuwa hali hiyo inachangiwa na ukosefu wa imani sahihi ya dini. Hata katika nchi tajiri kama Marekani, bado changamoto ya furaha kwa wananchi wake imeendelea kuwepo.

Mmoja wa wanafalsafa wa Kimarekani aliwahi kusema: "Maisha katika jiji la New York ni pazia zuri linalofunika hali halisi ya huzuni na mateso."

KALAMU HURU

SEHEMU YA 6

SHEIKH Shaaban Mussa
0786 272 323

# Sadaka na ukarimu – roho ya kijamii baada ya Ramadhan

Mwezi wa Ramadhan si tu ulikuwa mwezi wa ibada za binafsi kati ya mja na Mola wake, bali pia ulikuwa ni mwezi wa kuimarisha uhusiano kati ya watu katika jamii.

Ndani ya mwezi wa Ramadhan, moyo wa Muislamu ulikuwa laini mno, huruma ziliongezeka, na mikono ilikuwa tayari zaidi kutoa na kusaidia wengine.

Ni katika Ramadhan ambapo tulishuhudia watu wakitoa sadaka kwa wingi, wakisaidia maskini, wakigawa vyakula vya futari, na kujitolea kwa hali na mali. Hii inaonesha wazi kwamba Ramadhan ilikuwa shule au chuo kweli cha ukarimu na huruma.

Mwenyezi Mungu amesema: "Mfano wa wanaotoa mali zao katika njia ya Mwenyezi Mungu ni kama chembe iliyoota mashuke saba, katika kila shuke kuna nafaka mia; na Mwenyezi Mungu humzidishia amtakaye." [Qur'an, 2: 261].

Lakini swali muhimu ni hili, je, ukarimu ule unaendelea hata baada ya Ramadhan kuisha?

Sadaka ni nini? Ni kutoa sehemu ya mali yako au uwezo wako kwa ajili ya kuwasaidia wengine kwa kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu.

Sadaka haishii kwenye mali pekee, bali inajumuisha hata tabasamu, msaada wa aina yoyote, au neno jema. Mtume (Allah amshushie rehema na amani): amesema: "Tabasamu lako kwa ndugu yako ni sadaka."

Ndani ya Ramadhan, Muislamu alihisi kwa undani zaidi maumivu ya njaa na kiu. Hali hii ilimfanya awe karibu zaidi na wale wanaoishi katika hali ngumu za maisha kila siku. Hivyo, moyo wake husukumwa kutoa ili kupunguza mateso ya wengine.

Hii ni hekima kubwa ya funga; ililenga kumjenga Muislamu asiwe mbinafsi, bali awe mtu wa kujali na kushirikiana na wengine.

Baada ya Ramadhan, changamoto ni kudumisha moyo huu wa ukarimu. Kwa baadhi ya watu, sadaka hupungua au hata kusimama kabisa. Hii ni ishara kwamba mafunzo ya Ramadhan hayakujikita kikamilifu.

Muislamu anatakiwa kuelewa kwamba kusaidia wengine si ibada ya msimu, bali inapaswa kuwa sehemu ya maisha yake ya kila siku. Jamii yenye mshikamano na amani hujengwa na watu wanaojali na kusaidiana.

Miongoni mwa njia za kudumisha ukarimu baada ya Ramadhan ni kujipangia kiwango maalum cha kutoa sadaka mara kwa mara, hata kama ni kidogo. Kidogo cha kudumu kina baraka kubwa zaidi kuliko kikubwa kinachokatika.

Na Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Amali zinazopendwa zaidi na Mwenyezi Mungu ni zile za kudumu, hata kama ni chache."

Aidha, Muislamu anaweza kuchangia kwa njia mbalimbali kulingana na uwezo wake. Wenye mali wanaweza kutoa fedha, kulipia matibabu, kulipa ada au kutoa chakula, na wasio na mali wanaweza kutoa muda wao, nguvu zao, au hata elimu yao kwa ajili ya kuwasaidia wengine.

Vilevile, ni muhimu kusaidia watu wa karibu kwanza; familia, majirani, na jamii inayokuzunguka. Hii hujenga mshikamano na kuimarisha mahusiano ya kijamii.

Mwenyezi Mungu amesema: "Chukua sadaka katika mali zao ili uwatakase na uwasafishe kwayo." [Qur'an, 9: 103]. Hii ina maana, moja ya faida kubwa ya sadaka ni kusafisha moyo dhidi ya ubahili, husda na chuki. Mtu anapotoa, moyo wake huwa mwepesi na hujaa furaha.

Pia, sadaka huondoa msongo, huleta baraka katika mali na maisha kwa ujumla. Aidha, sadaka ni kinga dhidi ya majanga na matatizo. Ni mlango wa riziki na sababu ya kupata rehema za Mwenyezi Mungu.

Mtume (Allah amshushie rehema na amani zimshukie) amesema: "Mali haipungui kwa sababu ya sadaka." Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Sadaka huipoza dhambi kama maji yanavyozima moto."

Ni muhimu pia kwa Muislamu kutoa sadaka kwa nia safi, si kwa kujionesha au kutafuta sifa za watu. Lengo kuu linapaswa kuwa ni kupata radhi za Mwenyezi Mungu na kusaidia viumbe Wake.



Kwa hakika, ukarimu ni sifa ya watu wema. Na Muislamu aliyefundishwa vema na Ramadhan anapaswa kuwa kielelezo cha huruma na upendo katika jamii yake.

Hivyo basi, baada ya Ramadhan, kila mmoja wetu anapaswa kujiuliza, je, bado ninatoa kama nilivyokuwa natoa ndani ya Ramadhani? Je, moyo wangu bado una huruma kwa wengine?

Lakini pamoja na kutoa mali na kusaidia wengine, kuna jambo jingine muhimu sana ambalo Ramadhan hulijenga kwa kina ndani ya nafsi ya Muislamu, nalo ni kumkumbuka Mwenyezi Mungu mara kwa mara.

Katika makala inayofuata, tutazungumzia kuhusu Dhikri (Kumkumbuka Mwenyezi Mungu) kama njia ya kudumisha uhai wa moyo baada ya Ramadhan, na jinsi ya kuendeleza mazoea ya kumtaja Allah katika maisha ya kila siku.

ذُوالقِعدة

MAKALA MAALUM

SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

# Je, Waislamu wanachagua riwaya zinazowafaa tu? Mfano wa kisa cha Bi Aisha

**Kumeibuka mijadala ya kidini mitandaoni ambapo mara nyingi wasio Waislamu hudai kuwa Waislamu "huchagua" riwaya wanazozipenda, wanazozikubali na zinazomsifu Mtume wao, na wanazikataa zile zinazoleta utata.**
**Hoja hii juu juu inaonekana kuwa na nguvu, lakini inapochambuliwa kwa kina, inaacha mapengo makubwa ya kielimu. Ili kuielewa vizuri, ni lazima kuangalia misingi ya uchambuzi wa riwaya ndani ya Uislamu pamoja na mtazamo wa sayansi ya baiolojia.**

Kwanza kabisa, ndani ya Uislamu kuna taaluma maalum iitwayo Ilmu al-Hadith. Hii ni sayansi iliyojengwa kwa karne nyingi kwa lengo la kuchuja na kuthibitisha riwaya zinazomhusu Mtume.

Tofauti na dhana ya baadhi ya wakosoaji, mfumo huu haujajengwa juu ya hisia bali juu ya kanuni madhubuti zinazofanana kwa kiasi kikubwa na mbinu za kisasa za uchunguzi wa taarifa. Wanazuoni huangalia mlolongo wa wapokezi (isnad), uadilifu wao, uwezo wao wa kuhifadhi kumbukumbu, pamoja na maudhui ya riwaya yenyewe (matini).

Ikiwa riwaya inapingana na Qur'an au ukweli uliothibitishwa, basi huchunguzwa kwa makini zaidi au hata kukataliwa.

Kwa msingi huo, si sahihi kusema kwamba Waislamu wanakubali riwaya kwa sababu zinawasifia. Mfano maarufu ni kauli ya Aisha bint Abubakr (Allah amridhie), kwamba "tabia ya Mtume ilikuwa Qur'an." Riwaya hii imekubaliwa si kwa sababu ni ya sifa, bali kwa sababu imekidhi vigezo vya uhakiki: ina wapokezi wanaoaminika na haipingani na Qur'an yenyewe, ambayo pia inamsifu Mtume kwa tabia njema.

Hata hivyo, mjadala mkali huibuka linapokuja suala la umri wa Aisha wakati wa ndoa. Baadhi ya riwaya, hasa zile zilizoandikwa katika vitabu kama Sahih al-Bukhari, zinaeleza kuwa aliolewa akiwa na miaka sita na akaanza kuishi na mumewe akiwa na umri wa miaka tisa. Wanazuoni wengi wa kale walizikubali riwaya hizi kwa sababu ya nguvu ya mlolongo wa wapokezi wake. Lakini hili halimaanishi kuwa ndio kusiwe na mjadala.

Kwa kweli, kuna uchambuzi wa kihistoria unaohoji uelewa huo wa umri. Kwa mfano, dada yake Aisha, Asma bint Abubakr, anaripotiwa kuwa alikuwa mkubwa kwa takriban miaka kumi na alifariki akiwa na umri wa miaka 100 mwaka 73 Hijriya. Hesabu hii inaashiria kuwa Aisha angeweza kuwa na umri mkubwa zaidi kuliko ule unaotajwa katika baadhi ya riwaya.

Aidha, kuna dalili kuwa Aisha alikumbuka na kuelewa matukio ya mwanzo ya Uislamu kwa kiwango kinachoashiria ukomavu fulani wa kimwili na kiakili, si utoto mdogo kabisa. Hapa tunaona wazi kuwa si suala la "kukataa kwa sababu ni baya," bali ni mjadala halali wa kielimu unaotumia vyanzo mbalimbali vya historia.

Kutoka upande wa baiolojia, mjadala huu unahitaji kuwekwa katika muktadha sahihi wa kisayansi. Ndani ya Biology, hasa katika tawi la Human Development, kipimo muhimu cha ukomavu wa kijinsia si namba ya miaka bali kufikia hatua ya Puberty, yaani balehe. Hapa ndipo mwili wa binadamu huwa na uwezo wa uzazi. Ni ukweli pia kwamba umri wa kufikia balehe hutofautiana kulingana na mazingira, lishe na hali ya kijamii. Katika jamii za kale, tofauti hizi zilikuwa kubwa zaidi kuliko ilivyo leo.

Ni muhimu pia kufafanua kuwa neno "pedophilia" lina maana maalum katika Psychiatry, linahusu mvuto wa kingono kwa watoto ambao hawajafikia balehe. Hivyo kulitumia moja kwa moja kwa matukio ya kihistoria bila kuchunguza hali ya kibaiolojia ni kutoa majibu mepesi mno yasiyoambatana na utafiti wa kina kwenye suala nyeti na tata kama hili.

Hoja nyingine inayotolewa ni kuhusu simulizi za Mitume waliotangulia, kama Suleiman, kupewa uwezo juu ya upepo. Hili kwa Waislamu si jambo la kubishaniwa, kwani limetajwa wazi ndani ya Qur'an. Kinachoweza kukataliwa ni maelezo ya ziada yasiyo na uthibitisho madhubuti, kama simulizi za "mkeka unaoruka," ambazo mara nyingi hutokana na riwaya dhaifu au tafsiri zisizo na msingi imara. Hapa tena tunaona matumizi ya kanuni ile ile ya uchambuzi, si kila simulizi ina uzito sawa.

Kwa mtazamo mpana, hoja ya mkosoaji inafanana na kudhani kuwa vyanzo vyote vina thamani sawa. Lakini hata katika Scientific Method, tafiti hutofautiana kwa ubora. Utafiti mmoja unaweza kuwa na ushahidi thabiti na mwingine dhaifu, na matokeo yake hupimwa kwa viwango tofauti. Vivyo hivyo, katika Ilmu al-Hadith, riwaya hupimwa, kuchunguzwa, na kupewa daraja kulingana na nguvu yake ya ushahidi.

Kwa hiyo, hitimisho la mada hii ni wazi: madai kwamba Waislamu wanachagua riwaya wanazozipenda ni tepetevu mno na hayazingatii mifumo ya kina ya kielimu iliyopo.

Ukweli ni kwamba kuna utaratibu makini wa kuchambua riwaya, mjadala halali wa kihistoria kuhusu masuala yenye utata, na uelewa wa kisayansi unaohitaji kuzingatiwa kabla ya kutoa hukumu nzito. Huu ndio mtazamo wa kina unaoweza kujibu hoja kama hizi bila jazba, bali kwa ushahidi na mantiki.

ذوالقعدة

# فتاوى



**SHEIKH**
**Shaaban Mussa**
**0786 272 323**

## Swali: Sheikh, ni nini kafara ya au adhabu ya mtu aliyemuita mkewe "mama"?

**Jibu:** Hiyo inaitwa Dhwihar, ikimaanisha kitendo cha mwanaume kumwambia mke wake maneno kama "Wewe ni kama mama yangu" kwa nia ya kumfananisha naye ili kujiepusha naye kimapenzi. Hii ilikuwa ni desturi ya zama za ujinga (jahiliyyah) na Uislamu uliikataza tabia hii.

Allah kwenye Qur'an (58:2–4) ameweka wazi kuwa kauli hii ni kosa kubwa lakini haivunji ndoa moja kwa moja bali inahitaji kafara kabla ya kurudi kwa mke kimwili.

Aya hizo zinasema: "Wale miongoni mwenu wanaowatenga wake zao, hao si mama zao. Hawakuwa mama zao isipokuwa wale waliowazaa. Na hakika hao wanasema neno linalochusha, na la uongo. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kughufiria, Mwenye kusamehe. Na wale wanaojitenga na wake zao, kisha wakarudia yale waliyoyasema, basi wamkomboe mtumwa, kabla hawajagusana...."

### Mpangilio wa kafara wa dhwihar na masharti

Mpangilio wa kafara ya dhwihar kwanza, kumuacha huru mtumwa; lakini kama hawezi basi atatakiwa kufunga miezi miwili mfululizo bila kukatiza. Ikitokea kuwa hawezi yoyote kati ya mawili hayo, kumkomboa mtumwa au kufunga miezi miwili; basi alishe maskini 60.

Pia kuna masharti kadhaa ya dhwihar. Kwanza, kwa aliyefanya dhambi ya dhwihar haruhusiwi kurudi kwenye mahusiano ya ndoa kabla ya kafara. Pili, kitendo hicho cha dhwihar ni dhambi, hivyo inahitaji pia toba ya kweli. Iwapo ilisemwa bila nia ya dhwihar, hukumu inaweza kutofautiana kwa wanazuoni.

Na Allah ndiye Mjuzi zaidi

## Swali: Je, inajuzu kwa mtu anayekula nguruwe kumchangia damu Muislamu anayehitaji damu?

**Jibu:** Ndiyo, inajuzu kwa mtu anayekula nguruwe kuchangia damu kwa Muislamu anayehitaji katika dharura ya kitabibu au kuokoa maisha.Kuna sababu kadhaa ya hukumu hii. Kwanza, kula nguruwe ni haramu kwa Muislamu, lakini hilo halifanyi damu ya mtu huyo kuwa haramu kwa matumizi ya kitabibu.

Msingi wa hoja hapa ni kanuni ya fiqh: "Dharura huondoa uharamu" (adh-dhwarurat tubiḥu al-maḥdhurat). Sababu nyingine ni kuwa uhai wa binadamu una thamani kubwa sana katika Uislamu.

Hata hivyo, kuna masharti ya kuzingatiwa kwenye kuchangiana damu. Kwanza, damu iwe salama kiafya (isiwe na maambukizi).

Sharti la pili ni kuwa itumike kwa matibabu halali au kuokoa maisha. Vilevile, sharti la tatu, ikiwezekana, Muislamu mwenye afya awe wa kwanza kuchangia, lakini si sharti la lazima.

Kwa kutimisha, inaruhusiwa kuchukua damu ya mtu yeyote aliye salama kiafya kwa ajili ya matibabu, bila kujali anachokula. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

## Swali: Katika msikiti wetu hukusanyika watu kutoka maeneo mbalimbali kwa ajili ya swala, desturi iliyozoeleka ni kuwa mtu anapokusudia kufanya harusi, huwajulisha watu kuhuus jambo hilo msikitini baada ya Swala. Je, jambo hili linaruhusiwa?

**Jibu:** Hatuoni ubaya wowote katika hilo. Hiii haiingii katika kutangaza kitu kilichopotea (kama ilivyokatazwa msikitini), bali ni mwaliko wa kushuhudia ndoa na chakula (walima). Ikumbukwe kama hili lilitokea katika zama za Mtume (Allah amshushie rehema na amani). Baadhi ya Maswahaba (Allah awaridhie) walimtumia mwaliko, naye akawaambia waliokuwepo: "Nendeni kwa fulani, anawaiteni kwenye chakula." Pia, Mtume hakukemea kitendo hicho.

Pia, Abu Twalha alimtuma Anas siku moja kumwalika Mtume (Allah amshushie rehema na amani) kwenye walima, naye akawaambia waliokuwepo: "Simameni twendeni kwenye mwaliko wa Abu Twalha."

Kwa hiyo, kwa ushahidi huo, jambo hili halina ubaya. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

## Swali: Imamu anayetusalisha swala ya Ijumaa hasomi isipokuwa Suratul Ghaashiyah na Al-A'laa tu. Je, kitendo hiki ni sahihi? Na je, mnampa nasaha gani kuhusu hilo?

**Jibu:** Kitendo chake hicho ndio Sunna, kwani Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alisoma: "Sabbihisma Rabbikal A'laa" (Al-A'laa) katika rakaa ya kwanza ya Ijumaa, na akasoma pia Al-Ghaashiyah. Inafaa pia wakati mwingine kusoma sura nyingine, kama vile Al-Jumu'ah na Al-Munaafiquun, kwani Mtume pia alizisoma katika Swala ya Ijumaa.

Kwa ujumla, Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alipata kusoma sura kwa mipangilio aina tatu: Mosi, A'laa katika rakaa ya kwanza na Ghaashiyah katika ya pili (baada ya Al-Faatiha). Pili, alisoma Al-Jumu'ah katika ya kwanza na Al-Munaafiquun katika rakaa ya pili. Tatu, Al-Jumu'ah katika rakaa ya kwanza na Al-Ghaashiyah katika rakaa ya pili.

Kwa hiyo, ilivyothibiti kutoka kwake sura hizi kwa aina mbalimbali, si kushikilia moja tu kila mara. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

ذُو القِعدة

MAKALA MAALUM

SEHEMU YA 1

Na Said Rajab
0783 650 803

# Kwanini Ulaya wamekataa kushirikiana na Trump?



Kabla ya kuchunguza ugumu wa msimamo wa Ulaya kukataa kujiunga na Marekani katika vita yake dhidi ya Iran, ni muhimu kutazama nyuma kidogo ili kuelewa hali hiyo kupitia lenzi ya 'fundisho la Trump', ambalo limebadilisha dhana ya sera ya kigeni ya Marekani.

Maneno ya Rais Trump hayakuwa kauli mbiu za kampeni tu, bali yalikuwa ujumbe mzito kwa wapinzani na washirika wa Marekani. Tamaa zisizozuilika za kutawala uchumi na jiografia zilijitokeza wazi, kuanzia kudokeza kuinunua Gaza ili kuibadili kuwa sehemu ya miradi mikubwa ya burudani na uchumi, hadi mawazo ya ajabu ya kuitwaa Canada ili iwe jimbo la 51 la Marekani, au kununua kisiwa cha Greenland.

Matarajio haya hayakuhusu tu upanuzi wa kijiografia, bali pia yalikuwa pigo kwa moyo wa uhuru wa Ulaya, hasa ikizingatiwa kuwa Canada na Greenland zimefungamana kiutawala, kijiografia na kisiasa na duara la ushawishi wa Ulaya.

Hali hii iliambatana na vitisho vya wazi vya kujiondoa katika NATO, ambapo Ulaya imekuwa ikionekana kama mnufaika pekee, huku kiasi kikubwa cha fedha kikitozwa kwa Ukraine kama mbadala wa msaada wa kijeshi au kwa ajili ya kudhibiti madini yake adimu (REEs).

Mwenendo huu, uliotegemea shinikizo la kiuchumi na utozaji ushuru unaozidi asilimia 200 ulisababisha dharau na chuki miongoni mwa viongozi wa dunia, hasa washirika wakuu wa Marekani kama Uingereza.

Mataifa hayo yalijikuta yakikabiliwa na utawala unaofanya mambo kwa kiburi, huku Israel ikionekana kama mtoto anayedekezwa ambaye matakwa yake hutimizwa bila kuhojiwa.

Kiburi cha Marekani chini ya Donald Trump kimefikia viwango vya kutisha katika historia, kikibadili utawala wa nchi hiyo kuwa kama shirika la kimataifa linaloweka kanuni za maadili duniani, kinyume na sheria za kimataifa na kanuni za kidiplomasia.

Hali hii imechangia kuvunjika kwa utaratibu wa kimataifa ulioanzishwa baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia.

Kufuatia vita vya siku 700 huko Gaza, Trump alitangaza kuanzishwa kwa 'Bodi ya amani' ya dunia kama mbadala wa Umoja wa Mataifa na Baraza lake la Usalama, akidai kuwa taasisi hizo zimepitwa na wakati.

Mwelekeo wa utawala wake ulijikita zaidi katika mafundisho ya Monroe (Monroe Doctrine), ukizuia uingiliaji wowote wa kimataifa katika masuala ya Marekani kutoka ng'ambo ya Atlantiki.

Hali hiyo ilijidhihirisha wakati Marekani ilipoivamia Venezuela, ikamkamata na kumdhalilisha Rais wa nchi hiyo ya Amerika ya Kusini, Nicolas Maduro, na kudhibiti kikamilifu sekta ya mafuta ya Venezuela. Vitendo hivyo vilifungua njia ya shambulio kubwa Mashariki ya Kati dhidi ya Iran.

Mpango wa Marekani ulijikita katika mkakati wa siku nne, yaani kufanya shambulio la ghafla na kali kama radi, ambalo lingewaangamiza viongozi wa ngazi ya juu wa Iran, akiwamo Kiongozi Mkuu, ili kuilazimisha nchi hiyo kujisalimisha ndani ya saa 96.

Dhamira ilikuwa kufanikisha kaulimbiu ya 'Marekani Kwanza' kwa kunyakua udhibiti wa Mashariki ya Kati pamoja na rasilimali zake kubwa za mafuta, gesi na madini adimu ya ardhini (REEs), pamoja na kudhibiti milango ya bahari na njia kuu za majini ambazo ni mhimili wa biashara ya kimataifa.

Mafanikio ya Marekani katika mkakati huo yangethibitisha utabiri wa aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Dkt. Henry Kissinger, pamoja na Prof. Zbigniew Brzezinski, gwiji wa sera ya mambo ya nje wa Marekani, kwamba yeyote anayedhibiti Mashariki ya Kati anadhibiti dunia na huwa kiongozi asiye na mpinzani.

Hata hivyo, mikakati iliyopangwa kwa miongo kadhaa na kutekelezwa kwa uangalifu mkubwa inaweza kukumbwa na matokeo yasiyotarajiwa kutokana na kiburi cha nguvu kubwa.

Marekani ilipitisha mkakati wa mashambulizi ya kushtukiza ili kumvuruga na kumdhoofisha adui yake, lakini Iran haikutikiswa na mashambulizi ya awali.

Badala yake, ilijibu kwa haraka na kwa nguvu ikitumia makombora ya 'ballistic' na 'hypersonic' na kuharibu vituo vingi vya kijeshi vya Marekani vilivyopo Mashariki ya Kati. Pia iliishambulia vikali Israel, mshirika mkuu wa Marekani na kusababisha uharibifu mkubwa.

***Itaendelea wiki ijayo, Insha Allah***

TUJIFUNZE

AI (ARTIFICIAL INTELLIGENCE)

Na Junaynat Ally Dama

# Mbinu chache za uundaji wa maelekezo kwa AI ili upate utakacho




Katika matumizi ya kisasa ya akili mnembe (AI), wengi hufikiri kuwa teknolojia yenyewe ndiyo huamua ubora wa majibu.

Lakini ukweli ni tofauti: ubora wa matokeo unategemea zaidi namna swali linavyoulizwa kuliko uwezo wa mfumo wenyewe. Hapa ndipo dhana ya uundaji wa maelekezo (prompt engineering) inapopata umuhimu wake—sanaa na mbinu ya kuunda maelekezo sahihi ili kupata majibu bora.

Kuna mambo kadhaa muhimu ya kujua katika hili.

Mosi, uundaji wa maelekezo kwa AI ni suala la uwazi wa mawazo, si ugumu wa maneno. Watu wengi huamini kuwa ili kupata majibu bora kutoka kwa AI wanahitaji kutumia lugha ngumu au istilahi za kiufundi.

Kinyume chake, utafiti unaonyesha kuwa kinachohitajika ni kueleza kwa uwazi kile unachotaka. Swali lisiloeleweka humlazimisha mfumo kubahatisha, na matokeo yake huwa majibu ya jumla au yasiyolenga hitaji halisi.

Pili, umuhimu wa uundaji wa maelekezo unatokana na jinsi AI inavyofanya kazi. Mfumo wa AI huchagua majibu yake kulingana na taarifa anazopewa. Hivyo, kama maelekezo hayana mwelekeo, mfumo unaweza kutoa majibu mengi yanayowezekana lakini si lazima yawe sahihi au yanayokusudiwa. Kwa hiyo, tofauti kati ya majibu mazuri na mabaya mara nyingi si uwezo wa AI, bali ubora wa swali.

Tatu, kuongeza muktadha (context) hubadilisha kabisa ubora wa majibu. Swali kama "eleza AI" linaweza kutoa majibu ya jumla sana. Lakini unaposema "eleza AI kwa mwanafunzi wa mwaka wa kwanza wa chuo kwa maneno rahisi," unampa mfumo mwongozo wa hadhira, kiwango na mtindo wa maelezo. Hii huondoa utata na kuongeza usahihi wa majibu.

Nne, kuweka mipaka (constraints) ni sehemu muhimu ya prompt nzuri. Bila mipaka, AI inaweza kutoa majibu marefu kupita kiasi au yasiyo na mwelekeo. Mipaka inaweza kuwa urefu wa jibu, mtindo wa uandishi, au hata muundo wa majibu. Kwa kufanya hivyo, unabadilisha AI kutoka kuwa chombo cha jumla hadi kuwa mshirika maalum wa kazi.

Tano, kugawanya kazi ngumu katika hatua ndogo huongeza ubora wa matokeo. Badala ya kuuliza swali moja kubwa, ni bora kulivunja katika sehemu ndogo zinazoeleweka. Njia hii huruhusu mfumo kushughulikia kila kipengele kwa utaratibu, na matokeo yake huwa yaliyopangwa vizuri na rahisi kueleweka.

Sita, kueleza mtazamo au jukumu la AI kunabadilisha kabisa namna jibu linavyotolewa. Unaposema "andika kama mwalimu," "andika kama mchambuzi," au "andika kama mwandishi wa habari," unaunda muktadha wa sauti, mtindo na kina cha maelezo. Hii inaifanya AI kuwa zaidi ya chombo cha majibu—inaifanya kuwa mshirika wa kitaaluma.

Saba, matumizi ya uundaji wa maelekezo yana athari kubwa katika maisha halisi. Katika uandishi wa maudhui, huwezesha kuandika makala, ripoti au muhtasari unaolenga hadhira maalum bila marekebisho mengi.

Katika elimu, husaidia kueleza dhana ngumu kwa lugha rahisi au kwa mifano inayoeleweka. Katika programu (coding), huwezesha kupata suluhisho sahihi kwa matatizo ya kiufundi kwa muda mfupi.

Nane, bila ujuzi wa uundaji wa maelekezo, AI inaweza kuonekana kama chombo kisichoaminika. Watumiaji wengi hulazimika kurekebisha maswali mara kwa mara au kupata majibu yasiyofaa. Hii husababisha kupoteza muda na kuleta hisia kwamba mfumo hauna uwezo. Lakini mara nyingi tatizo si mfumo bali namna ya kuuliza.

Tisa, uundaji wa maelekezo ni ujuzi unaoongeza tija. Badala ya kutumia muda mwingi kurekebisha majibu, mtumiaji hupata matokeo sahihi kutoka mwanzo. Hii inaifanya AI kuwa chombo cha vitendo zaidi katika kazi za kila siku—kuanzia utafiti hadi mawasiliano ya kitaaluma.

Kumi, kwa mtazamo mpana, uundaji wa maelekezo ni daraja kati ya binadamu na teknolojia. Inahakikisha kuwa kile tunachofikiria kinaweza kueleweka na mfumo wa AI kwa usahihi. Kadri teknolojia inavyoendelea, ujuzi huu unakuwa muhimu zaidi, si kwa wataalamu wa teknolojia pekee bali kwa kila mtu anayehitaji kutumia AI kwa ufanisi.

ذوالقعدة

MUSSA IMANI SHEHA ZANZIBAR
0773 181 494

SEHEMU YA 5



# SIMULIZI YA MTUME MUSA (AMANI YA ALLAH IMSHUKIE)

## VISA VYA MITUME NA MASWAHABA

**Makala yetu katika toleo lililopita ilitufikisha pale Mtume Musa alipojitolea kuwasaidia mabinti wawili walioshindwa kupigana vikumbo na wachungaji wengine na wakaamua kukaa pembeni kusubiri mpaka wengine wamalize kunywesha.**
**Tuliona kuwa Musa (amani ya Allah imshukie), baada ya kutoa msada ule, alirudi kivulini na kwa unyenyekevu na kwa yakini pevu akamuomba Mola wake amshushie kheri (ufumbuzi) kutokana na shida aliyonayo na amuhifadhi huko ugenini alipo.**

### Mabinti warudi nyumbani

Mabinti walipofika nyumbani, baba yao aliwauliza: "Mbona leo mmerudi mapema hivi?" Wakajibu: "Allah ametuletea mtu mwema na mkarimu akatusaidia."

Baba akastaajabu sana na kuwauliza: "Mtu gani huyo na mmemuacha wapi?" Wakajibu: "Tumemuacha kule kule kisimani, na inaonekana ni mtu mgeni hana jamaa (mwenyeji)."

Baba alitafakari na kusema kimoyomoyo: "Mtu mgeni aliyetufanyia wema, ukifika usiku ataenda na kupumzikia wapi? Bila shaka tuna wajibu wa kumuita hapa na kumkirimu (kumlipa) kwa wema wake." Kisha akamuarisha mmoja wa binti zake aende akamuite huyo mgeni.

Qur'an inasimulia: "Basi akamjia (Musa) mmoja katika wale wawili anakwenda na huku anaona haya, akasem, 'Baba yangu anakuita ili akulipe ujira wa kutunyweshea...'" [Qur'an, 28:25].

Hapo Musa (amani ya Allah imshukie) akajua kwamba Allah amemkubalia sadaka yake ya wema na maombi yake, kwa hiyo hakukataa wito. Kipengele hiki kinatufunza moja ya vipengele muhimu moja ya tabia ambazo mabinti wa Kiislamu wanatakiwa kujipamba nazo: aibu, hususan wanapoongea na wanaume.

Musa akatangulia ilhali binti huyo akimfuata kwa nyuma, lengo la kutangulia ni jicho lake lisione maumbile ya binti yule.

### Akutana na baba wa mabinti, apata ajira

Alipofika nyumbani kwa mabinti, baba alimuuliza jina, alikotoka na kisa cha kukimbilia pande hizo. Musa alijitambulisha kwa mzee huyo (mwema) na kumuhadithia mkasa wote kwa ukamilifu.

Mzee alisikiliza kwa utulivu na kwa umakini sana, alipomaliza akamtoa wasiwasi na kumkaribisha nyumbani. Tuirejee tena Qur'an: "... basi alipomfikia na kumsimulia kisa chote, alisema, 'Usiogope, umeshaokoka na watu madhalimu.'"

Musa aliishi katika nyumba ile kama mgeni mheshimiwa, na kushika nafasi ya kijana apendwaye na watu wake. Alizoea na alizoeleka.

Qur'an inasema: "Akasema mmoja wa wale (mabinti) wawili, 'Ewe baba yangu, mpe ajira huyu (awe anakuchungia wanyama wako badala yetu), bila shaka mbora wa uwezae kumuajiri ni mwenye nguvu muaminifu (na huyu ana sifa zote hizo).'"

Kipengele hiki katika simulizi ya Nabii Musa kinatufundisha umuhimu wa sifa za kuwa na nguvu, mkweli na muaminifu ili kupata ajira.

Nguvu za mwili na za kiroho humuwezesha muajiriwa kukabiliana na majukumu ya kazi za kila siku kwa ufanisi. Ukweli na uaminifu humjengea muhusika heshima, mapenzi na muamala mzuri kwa muajiri wake.

### Ajira na ndoa

Mzee aliwafiki rai ya binti yake na akaona ili kujenga mahusiano mazuri zaidi na Musa (muajiriwa wake), basi bora amuoze binti yake.

Mzee akamwambia Nabii Musa: "Mimi nataka nikuoze mmoja wa mabinti zangu hawa kwa kunitumikia miaka minane. Na kama ukitimiza kumi ni khiari yako, lakini mimi sitaki kukutaabisha, na utanikuta inshAllah ni miongoni mwa watu wema (watekelezao makubaliano)." [Qur'an, 28:27].

Haya ndio mahari aliyotakiwa kuyatoa Musa (amani ya Allah imshukie) ili apate mke. Ni utumishi wa kuchunga wanyama kwa miaka nane na kuhangaishana nao, lakini akipenda kukamisha kumi –kama hisani-sio vibaya.

Nabii Musa akakubali matakwa ya baba wa binti. Na dhahiri –na kwa mujibu wa wataalamu wengi wa tafsiri - inaonekana kwamba, walifunga mkataba wa ajira na ndoa pamoja. Kwa maana nyingine, walipopitisha makubaliano tu, Musa akawa tayari ameshamuoa yule binti, akaishi pale kama muajiriwa, huku pia akiwa mume wa mtu.

### Angalizo:

Kuna hitilafu kati ya wanazuoni wetu kuhusu suala la je, yule mwenyeji wa Musa kule Madyan ndiye Nabii Shuaibu aliyesimuliwa na Qur'an ama siye? Qur'an haikutaja jina lake lakini pale ndipo alipoishi (Shuaibu) na watu wake, kama tulivyoeshiria katika toleo lililopita.

Wapo waliosema kwamba, naam, yule alikuwa ni Shuabu mwenyewe (amani ya Allah imshukie), lakini wanazuoni waliokuja baadae wanasema kwamba, bwana mkubwa aliyefikiwa na Musa (amani ya Allah imshukie) na kumuozesha binti yake siye Nabii Shuaibu ambaye alitumwa na Allah kwe watu wa Madyan.

*Itaendelea inshaAllah*

ذو القعدة

MAKALA YA AFYA

Na Junaynat Ally Dama

# Kuanzia kizazi cha 2009 marufuku kununua tumbaku maisha yao yote

Kwa miaka mingi, kupitia sinema, matangazo na kazi nyingine za sanaa, tulifundishwa kimyakimya kwamba kuvuta sigara ni ishara ya ujanja, uhuru na hadhi. Mhusika mkuu akivuta, anaonekana mtulivu, mwenye kujiamini—karibu mfano wa kuigwa.

Sasa hali imegeuka. Wale waliotengeneza simulizi hiyo hiyo wanapiga marufuku sigara kwa kizazi kipya. Swali la moja kwa moja: sisi tulioiwaiga na kuona umagharibi ndo ujanja, tunafanya nini sasa?

Ni hivi: Uingereza imechukua hatua ya kihistoria kwa kupitisha sheria inayokataza kabisa uuzaji wa sigara kwa watu wote waliozaliwa kuanzia mwaka 2009. Ingawa hii sio marufuku ya kuvuta sigara, lakini bado ni hatua kuelekea kupunguza matumizi.

Kwa kifupi, kizazi hiki hakitaruhusiwa kununua tumbaku katika maisha yao yote. Serikali inalenga kujenga kile kinachoitwa "kizazi kisichovuta sigara"—jamii ambayo kwa muda mrefu itaondokana na uraibu huu unaosababisha madhara makubwa ya kiafya.

Tofauti na marufuku za ghafla, sheria hii inafanya kazi kwa hatua: kila mwaka, umri wa kuruhusiwa kununua sigara unaongezwa. Hivyo, wale walio chini ya umri fulani leo hawatawahi kufikia umri wa kisheria wa kununua tumbaku. Hii ni mbinu ya kimkakati ya muda mrefu inayolenga kuondoa sigara taratibu hadi zipotee kabisa.

Lakini zaidi ya taarifa ya habari, hatua hii ina maana pana zaidi—hasa inapochunguzwa kwa mtazamo wa afya ya umma na maadili ya Kiislamu.

## Kwanza: Hoja ya afya na uchumi wa taifa

Kwa miongo kadhaa, uvutaji sigara umeendelea kuwa moja ya visababishi vikuu vya vifo vinavyoweza kuzuilika duniani. Magonjwa kama saratani ya mapafu, magonjwa ya moyo, na matatizo ya mfumo wa upumuaji yanahusishwa moja kwa moja na tumbaku.

Hata hivyo, hoja yenye uzito zaidi si vifo pekee—ni gharama. Serikali nyingi, ikiwemo ya Uingereza, zinatumia mabilioni ya fedha kila mwaka kugharamia matibabu ya magonjwa yanayosababishwa na sigara. Hizi ni fedha za walipa kodi ambazo zingeweza kuelekezwa kwenye maendeleo mengine: elimu, miundombinu, au huduma za kijamii.

Kwa mantiki hii, marufuku ya kununua sigara si tu hatua ya kiafya, bali pia ni sera ya kiuchumi. Inazuia mzigo wa kifedha kabla haujatokea. Ni sawa na kuziba uvujaji kabla maji hayajaharibu nyumba yote.

Aidha, ushahidi unaonyesha kuwa watu wengi huanza kuvuta sigara wakiwa vijana. Kwa kuzuia mwanzo huo, serikali inakata mnyororo wa uraibu mapema—na hivyo kupunguza kwa kiasi kikubwa idadi ya wagonjwa wa baadaye.

## Pili: Mtazamo wa Kiislamu—kulinda maisha ni wajibu

Katika Uislamu, uhai wa binadamu ni amana kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Qur'an inaweka wazi kanuni hii kwa kusema: "Wala msijiue wenyewe..." [4: 29]. Aya hii si tu kuhusu kitendo cha ghafla cha kujiua, bali pia inajumuisha vitendo vinavyopelekea uharibifu wa mwili taratibu.

Kwa lugha rahisi, uvutaji sigara ni aina ya kujidhuru polepole. Ni kuchagua kwa hiari kuingiza sumu mwilini kwa muda mrefu, huku madhara yake yakijulikana wazi. Ndiyo maana wanazuoni wengi wa Kiislamu wamehukumu uvutaji sigara kuwa haramu au angalau makruhu sana.

Uislamu pia unakataza israfu—matumizi mabaya ya mali. Fedha zinazotumika kununua sigara ni matumizi yasiyo na faida, na mara nyingi huambatana na gharama kubwa za matibabu baadaye. Hivyo, sigara huathiri si afya tu, bali pia uchumi wa mtu na jamii.

Zaidi ya hapo, kuna dhana ya maslaha ya umma (faida ya jamii). Sheria yoyote inayolenga kulinda maisha na kuzuia madhara makubwa inaendana na malengo ya juu ya Sharia (Maqasid al-Sharia), hasa kulinda uhai (hifz al-nafs).

## Changamoto kwa Waislamu

Ni muhimu pia kutambua kuwa hata serikali zisizo za Kiislamu zinaweka sheria kali walau kupunguza vitendo vya kujiua. Hii inaonyesha kuwa kulinda maisha si tu suala la dini, bali ni kanuni ya msingi ya ustaarabu wa binadamu. Kwa mantiki hiyo, marufuku ya sigara inaweza kueleweka kama hatua inayolingana na lengo hilo hilo—kuzuia madhara yanayoelekea kwenye kupoteza maisha.

Kuna hoja ya kujitafakari hapa. Mataifa ya Waislamu, ambayo yana mwongozo wa wazi wa kidini kuhusu kulinda afya na kuepuka madhara, yalikuwa na msingi wa kuchukua hatua kama hizi mapema zaidi. Sababu zilikuwepo: dalili za kisayansi, mafunzo ya dini, na athari za kijamii.

Moja ya sababu ya kigugumizi cha kuchukua hatua ni hofu ya kuonekana kuingilia maamuzi ya watu. Lakini kinachoshangaza ni kwamba leo, mataifa ambayo mara nyingi hujinasibu kwa kusisitiza uhuru wa mtu binafsi ndiyo yamechukua hatua kali zaidi.

ذو القعدة

**MATUKIO YENYE MAZINGATIO**

NA ZAHARANI BARAKA

# Ibada ya Hijja na wajibu wa mtoto kwa mzazi wake

**Imepokewa hadith kutoka kwa Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) kwamba siku moja wakati wa sherehe za Idd al–Adh'ha alikuwa juu ya mnyama wake, kisha akampandisha Al–Fadhl bin Abbas (Allah amridhie), ambaye Allah Ta'ala alimjaalia sura nzuri.**

**Wakati huo, Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) alikuwa akiwajibu watu mbalimbali maswali yao ya dini. Ghafla, akatokea mwanamke kutoka kabila la Khath'am, ambaye pia alikuwa mzuri wa sura.**

**Mwanamke huyo alimuuliza swali Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) huku Al–Fadhl akimtazama kutokana na uzuri wake. Mtume alipoona hivyo akaweka mkono wake kwenye kidevu cha Al–Fadhl na kuugeuza uso wake ili asiendelee kumtazama.**

**Mwanamke yule akasema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Hakika faradhi ya Hijja imewafikia waja wa Mwenyezi Mungu, na baba yangu ni mzee sana, hawezi kukaa sawa juu ya kipando; je, naweza kumhijia?" Mtume akamjibu: "Ndiyo (waweza kumhijia)."** ***[Imenukuliwa na Bukhari]***

## Mafundisho ya tukio hili:

Tukio hili linaonesha unyenyekevu mkubwa wa Mtume (rehema na amani zimshukie) alipompandisha kijana mdogo juu ya mnyama wake. Hii ni ishara kuwa hadhi au heshima ya kiongozi haishuki kwa kuwajali na kuwa karibu na vijana.

Uislamu unahimiza unyenyekevu bila kujali cheo au hadhi ya mtu. Allah Ta'ala anasema: "Na shusha bawa lako (unyenyekevu) kwa Waumini wanaokufuata." [Qur'an, 26:215].

## Nafasi ya wanazuoni katika jamii

Wanazuoni ndiyo warithi wa Mitume, hivyo wanapaswa kuwa karibu na jamii ili kutoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali ya dini. Jamii inapaswa kurejea kwa wenye elimu pale inapokumbana na mambo yasiyoeleweka ili kuepusha mkanganyiko katika ibada.

Allah Ta'ala anasema: "Basi waulizeni wenye elimu ikiwa nyinyi hamjui." [Qur'an, 16:43]. Naye Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) amesema: "Mwenye kutakiwa kheri na Mwenyezi Mungu humpa ufahamu katika dini." [Bukhari na Muslim].


## Kukemea uovu kwa hekima

Mtume alipoona Al–Fadhl anamtazama mwanamke hakumkemea kwa maneno makali, bali alimrekebisha kwa upole kwa kuugeuza uso wake. Hii ni ishara tosha kuwa marekebisho ya vitendo yanaweza kuwa bora zaidi kuliko maneno makali.

Mtume wa Allah ameelekeza: "Atakayeona uovu miongoni mwenu auondoe (aubadilishe) kwa mkono wake; kama hawezi (auondoe) kwa ulimi wake (yaani aukemee); na akishindwa, basi kwa moyo wake (achukie moyoni), na huo (kuona ubaya kisha kuunyamazia) ni udhaifu wa imani..." [Muslim].

Kitendo cha Al–Fadhl kugeuza uso wake kinaonesha umuhimu wa kuepuka kutazama mambo au vitu visivyofaa, ambavyo aghlabu huleta fitina. Njia bora ya kuulinda moyo ni kudhibiti viungo vya mwili.

Allah Mtukufu alisema kumwambia Mtume Muhammad: "Waambie waumini wanaume wainamishe macho yao na wahifadhi tupu zao..." [Qur'an, 24:30]. "Na waambie waumini wanawake wainamishe macho yao..." [Qur'an, 24:31].



## Ruhusa ya kumhijia mtu mwingine

Katika tukio hili, tumeshuhudia Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) akimruhusu mwanamke wa kabila la Khath'am kumhijia baba yake ambaye alikuwa kikongwe. Hii ina maana kuwa Uislamu unaruhusu kumhijia mtu mwingine kwa sababu zinazokubalika kisheria, kama vile uzee au ugonjwa.

Hata hivyo, anayeruhusiwa kumhijia mtu mwingine ni sharti yeye mwenyewe awe amehiji, kama ilivyofafanuliwa katika hadith ya Shubrumah (Allah amridhie).

## Kuwatendea wema wazazi wawili

Kitendo cha mwanamke wa kabila la Khath'am cha kutaka kumhijia baba yake kinaonesha umuhimu wa kuwahudumia wazazi, hasa katika mambo ya dini. Uislamu unasisitiza kuwatii na kuwahudumia wazazi wawili, hasa wanapokuwa dhaifu.

Allah Ta'ala anasema: "Na Mola wako ameamuru msimuabudu (yeyote) ila Yeye, na uwafanyie wema wazazi wawili..." [Qur'an, 17:23]. Pia Mtume amesema: "Radhi ya Mola ipo katika radhi ya mzazi, na hasira ya Mola ipo katika hasira ya mzazi." [Tirmidhi].

JUNAYNAT
ALLY DAMA

# Kama mwanao ana dalili hizi, ana kipaji cha hali ya juu



Watoto wenye vipaji vya juu mara nyingi hawajitambulishi kupitia alama za mitihani pekee, bali huonyesha ishara zao mapema kupitia tabia, lugha na namna wanavyofikiri.

Saikolojia ya ukuaji inaeleza kuwa "giftedness" si jambo la kukariri au kufaulu darasani tu, bali ni mchanganyiko wa kasi ya kufikiri, kina cha uelewa na nguvu ya kihisia. Hata hivyo, changamoto kubwa kwa wazazi na walimu ni kuzitambua ishara hizi mapema na kuzitafsiri kwa usahihi.

Mosi, watoto wenye vipaji huonyesha uwezo wa juu wa lugha mapema kuliko wenzao. Mtoto mdogo anayezungumza kwa sentensi ndefu, kutumia maneno ya watu wazima au kuelezea mambo kwa usahihi mkubwa, mara nyingi anaonesha ukuaji wa kiakili ulioharakishwa. Hii si bahati mbaya bali ni dalili ya ubongo unaofanya kazi kwa kasi na mpana zaidi.

Pili, huwa na udadisi usioisha. Maswali yao hayana mwisho, na mara nyingi hayaridhiki na majibu rahisi. Mtoto anayesema "kwa nini" mara kwa mara anaonyesha hamu ya kuelewa mantiki ya mambo, si kuyakubali tu. Udadisi huu ni msingi wa fikra huru na utafiti wa baadaye.

Tatu, watoto hawa mara nyingi wana kumbukumbu kali isiyo ya kawaida. Wanaweza kukumbuka maelezo madogo ya matukio yaliyopita, maneno waliyosikia au hata picha walizoona kwa muda mfupi. Uwezo huu wa kuhifadhi na kurejesha taarifa ni moja ya nguzo muhimu za maendeleo ya kitaaluma.

Nne, wana uwezo wa kufikiri kwa kina na kubaini mifumo au uhusiano wa mambo mapema. Badala ya kujifunza taarifa moja moja, wanaunganisha taarifa na kuona picha kubwa. Hii inaonekana katika uwezo wao wa kuelewa mifano, kejeli au hata dhana za kihisabati mapema kuliko wenzao.

Tano, huonyesha hisia kali pamoja na huruma ya juu. Mtoto anayehangaika kuhusu haki, mateso ya wengine au masuala ya kijamii anaweza kuonekana "mwenye hisia kupita kiasi," lakini kwa mtazamo wa saikolojia, hii ni ishara ya ufahamu wa kina wa kihisia na kijamii. Mara nyingi, watoto hawa hukua kuwa watu wenye uelewa mkubwa wa wengine.

Sita, maendeleo yao huwa hayalingani katika nyanja zote. Wanaweza kuwa na akili ya juu sana lakini wakawa na changamoto katika mambo ya kawaida kama uandishi au udhibiti wa hisia. Hali hii inajulikana kama asynchronous development, na mara nyingi huchanganya wazazi wanaotarajia ukuaji wa mtoto uwe sawa katika kila eneo.

Saba, wana ubunifu mkubwa na uwezo wa kufikiri nje ya mipaka ya kawaida. Watoto hawa hupenda kuuliza "vipi kama...?" na kuunda mawazo mapya, hadithi au suluhisho zisizotarajiwa. Huu ni msingi wa uvumbuzi na ubunifu wa baadaye.

Nane, wanapopenda jambo fulani, huonyesha umakini wa hali ya juu. Wanaweza kutumia muda mrefu wakijishughulisha na kitu kimoja bila kuchoka. Uwezo huu wa kuzingatia kwa kina ni rasilimali muhimu katika mafanikio ya kielimu na kitaaluma.

Tisa, mara nyingi huvutiwa na watu wakubwa kuliko wenzao. Badala ya kucheza tu na watoto wa rika lao, hupenda mazungumzo yenye maana au mijadala ya kina, jambo linaloendana na kiwango chao cha fikra.

Kumi, huonyesha unyeti mkubwa wa kihisia na kimazingira. Wanaweza kuguswa kwa urahisi na kelele, mwanga, au hata matukio ya kijamii. Ingawa hali hii inaweza kuonekana kama udhaifu, mara nyingi ni sehemu ya mfumo wao wa kiakili unaowapa uwezo wa ubunifu na huruma ya juu.

Kwa ujumla, kutambua vipaji vya mtoto kunahitaji macho ya kuona zaidi ya tabia za juu juu. Si kila mtoto ataonyesha dalili zote, lakini mchanganyiko wa ishara hizi huunda picha ya mtoto mwenye uwezo wa kipekee.

Changamoto kwa wazazi na walimu si kuharakisha ukuaji huu, bali kuusimamia kwa uangalifu—kwa kumpa mtoto changamoto zinazofaa, mazingira salama ya kihisia, na nafasi ya kucheza na kuchunguza dunia kwa uhuru.

ذوالقعدة

MAKALA
SAIKOLOJIA

UKHTI FATIMA SS

# Msongo wa mawazo wa wazazi unaathiri watoto kimya kimya

Katika maisha ya kila siku, wazazi wengi hukumbwa na changamoto nyingi—shinikizo la kazi, majukumu ya kifamilia, matatizo ya kifedha na majukumu mengine ya maisha. Mara nyingi msongo huu wa mawazo huonekana kama tatizo la watu wazima pekee. Hata hivyo, wataalamu wa saikolojia ya familia wanaonya kwamba msongo wa wazazi unaweza kuwa na athari kubwa kwa watoto, hata kama hauonekani wazi.

Kwa mujibu wa makala iliyochapishwa na The Times of India, watoto wana uwezo mkubwa wa kugundua mabadiliko ya kihisia kwa wazazi wao, hata kama wazazi hawajasema chochote kuhusu hali wanayopitia. Hii ina maana kwamba watoto wanaweza kuhisi mvutano, huzuni au uchovu wa wazazi wao kupitia sauti, mienendo au mazingira ya nyumbani.

## Watoto huhisi zaidi kuliko tunavyodhani

Kinyume na dhana kwamba watoto hawaelewi matatizo ya watu wazima, wataalamu wanasema watoto hutambua sana hali ya kihisia ya wazazi wao. Ingawa huenda wasielewe chanzo cha msongo huo, wanaweza kuhisi mabadiliko katika tabia au sauti ya mzazi.

Kwa mfano, mzazi mwenye msongo anaweza kuwa na haraka, kukosa uvumilivu au kuonekana hayupo kiakili wakati wa mazungumzo na mtoto. Hali hii inaweza kumfanya mtoto ahisi kuwa hapewi umakini au upendo wa kutosha.

## Watoto huiga hisia za wazazi

Tafiti nyingi za saikolojia zinaonyesha kuwa watoto mara nyingi huiga hali ya kihisia ya wazazi wao. Ikiwa mzazi anaonekana kuwa na wasiwasi au mkazo, mtoto anaweza pia kuanza kuonyesha dalili kama hizo.

Watoto wanaweza kuonyesha hali hii kwa njia mbalimbali. Baadhi wanaweza kuwa na wasiwasi zaidi, wengine kuwa wakorofi au wenye hasira, na wengine kujitenga kimya kimya. Mara nyingi wazazi huona mabadiliko haya katika tabia ya mtoto bila kutambua kwamba chanzo kinaweza kuwa msongo wao wenyewe.

## Hisia za usalama na athari za muda mrefu

Moja ya athari kubwa za msongo wa wazazi kwa watoto ni kupungua kwa hisia ya usalama. Watoto wanahitaji mazingira tulivu na yenye utulivu ili kujenga ujasiri na kujiamini. Wakati nyumba inajaa mvutano wa kihisia, mtoto anaweza kuanza kuhisi kwamba mazingira yake si salama kama alivyodhani.




Hali hii inaweza kuathiri namna mtoto anavyoshirikiana na wengine, jinsi anavyokabiliana na changamoto na hata uwezo wake wa kujifunza shuleni.

Wataalamu wa afya ya akili wanaeleza kuwa msongo wa muda mrefu katika mazingira ya familia unaweza kuathiri maendeleo ya kihisia na kiakili ya mtoto. Watoto wanaoishi katika mazingira yenye mvutano mara kwa mara wanaweza kupata matatizo kama wasiwasi, huzuni au matatizo ya tabia.

Hii haimaanishi kwamba kila mzazi anayepitia msongo atamdhuru mtoto wake. Badala yake, inaonyesha umuhimu wa kutambua jinsi hisia za wazazi zinavyoweza kuathiri mazingira ya familia.

## Nini wazazi wanaweza kufanya?

Habari njema ni kwamba hatua ndogo zinaweza kusaidia kupunguza athari hizi. Wataalamu wanashauri wazazi kujifunza mbinu za kudhibiti msongo kama kupumua kwa utulivu, kupumzika kwa muda mfupi au kuzungumza na mtu wanayemwamini.

Pia ni muhimu kwa wazazi kuwa wazi kwa watoto wao kwa kiwango kinachofaa umri wao. Badala ya kujificha kabisa, mzazi anaweza kusema kwa utulivu kwamba anahisi kuchoka au ana siku yenye shughuli nyingi. Hii humsaidia mtoto kuelewa hali bila kujihisi yeye ndiye chanzo cha tatizo.

Zaidi ya yote, wazazi wanashauriwa kujaribu kujenga mazingira ya mawasiliano ya wazi nyumbani. Watoto wanapohisi kuwa wanaweza kuzungumza na wazazi wao kuhusu hisia zao, wanakuwa na uwezo mkubwa wa kukabiliana na changamoto za kihisia. \Kwa ujumla, msongo wa wazazi ni sehemu ya kawaida ya maisha ya kisasa. Lakini kama ilivyoelezwa katika makala ya The Times of India, ni muhimu kutambua kwamba watoto wanaweza kuhisi mvutano huo hata kama hauonekani wazi.

Kwa kuzingatia afya ya kihisia ya wazazi na kujenga mazingira ya utulivu nyumbani, familia inaweza kuwa mahali salama ambapo watoto wanakua wakiwa na kujiamini, utulivu wa akili na mahusiano mazuri.



NA UKHTI FATIMA

# Mambo ya kuzingatia kwa wanaonza uwekezaji halal

**Katika enzi hii ya mabadiliko ya kifedha na teknolojia, watu wengi wanatafuta njia za kukuza mali zao bila kukiuka misingi ya maadili. Kwa Muislamu, swali si tu "niwekeze wapi?" bali "niwekeze vipi kwa njia halali?"**
**Uwekezaji halal, unaojulikana pia kama uwekezaji unaozingatia Shariah, unazidi kupata umaarufu duniani. Lakini kwa wanaoanza, mara nyingi huonekana mgumu au wenye masharti mengi. Ukweli ni kwamba, msingi wake ni rahisi—na unahitaji uelewa sahihi.**

## Uwekezaji halal ni nini hasa?

Kwa ufafanuzi wa msingi, uwekezaji halal ni kuweka fedha zako katika miradi au mali inayokubalika kwa mujibu wa sheria za Kiislamu. Hii inamaanisha kuepuka riba, kamari, na mikataba yenye utata mkubwa (gharar).

Lakini si suala la "kuepuka" tu—ni pia kuchagua. Uwekezaji halal unasisitiza uwekezaji katika shughuli halisi za kiuchumi kama biashara, viwanda, teknolojia au huduma. Hapa ndipo tofauti yake kubwa na baadhi ya mifumo ya kifedha ya kawaida inapojitokeza: faida lazima itokane na thamani halisi, si kubahatisha au mikataba ya kifedha pekee.

Kwa mtazamo mpana, huu ni mfumo unaochanganya uchumi na maadili—ndiyo maana hata wasiokuwa Waislamu wanauvutiwa kama aina ya uwekezaji unaowajibika kijamii.

## Kwa nini uwekezaji halal ni muhimu?

Sababu ya kwanza ni ya kiimani. Uislamu unasisitiza kipato halali, na uwekezaji ni sehemu ya kipato hicho. Hivyo, kuchagua uwekezaji halal ni sehemu ya ibada na utiifu.

Lakini pia kuna sababu za kiuchumi. Uwekezaji halal unaelekeza fedha katika shughuli halisi za uzalishaji, jambo linalochangia maendeleo ya uchumi. Aidha, kwa kuepuka kampuni zenye madeni makubwa, mara nyingi uwekezaji huu huwa na uthabiti zaidi katika nyakati za misukosuko ya soko. Kwa maneno mengine, ni mfumo unaojaribu kusawazisha kati ya faida na uwajibikaji.

## Kanuni kuu za uwekezaji halal

Ili kuanza kwa usahihi, ni muhimu kuelewa kanuni zake za msingi.

Kwanza ni marufuku ya riba. Mfumo wa Kiislamu haukubali faida inayotokana na kukopesha fedha bila kushiriki hatari ya biashara. Badala yake, unahimiza ushirikiano wa faida na hasara. Pili ni kuepuka sekta haramu. Hii ni pamoja na pombe, kamari, tumbaku na biashara zinazodhuru jamii.

Tatu ni kuepuka ubahatishaji na hatari zisizoeleweka. Uwekezaji unapaswa kuwa na uwazi na msingi wa mali halisi, si makubaliano ya kubahatisha. Kwa pamoja, kanuni hizi zinajenga mfumo unaolenga haki, uwazi na usawa katika shughuli za kifedha.

## Jinsi ya kuanza uwekezaji halal

Kwa anayeanza, hatua ya kwanza si kuweka fedha—ni kujifunza. Uwekezaji halal unahitaji uelewa wa kile unachowekeza na sababu zake.

Hatua inayofuata ni kuchuja (screening) uwekezaji. Hii inahusisha kuchunguza kampuni au mradi: je, unajihusisha na shughuli halali? Je, una kiwango kikubwa cha madeni ya riba?

Baada ya hapo, mwekezaji anaweza kuchagua njia inayomfaa. Wengine huanza na hisa za kampuni zinazokidhi vigezo vya Shariah, wengine huingia kwenye mifuko ya uwekezaji ya Kiislamu au majukwaa ya kidijitali yanayorahisisha uchambuzi wa uwekezaji halal.

Teknolojia imeanza kubadilisha uwanja huu. Sasa kuna programu na mifumo inayochuja hisa au uwekezaji kwa kutumia vigezo vya Shariah, jambo linalorahisisha sana kwa wawekezaji wapya.





"Afya"is natural source of sweet drinking water from underground stream which is blended with essential minerals to support and aid perfect metabolism.

WATERCOM LIMITED
P.o. Box 20409, Plot N.4005, Kisarawe11 area Temeke, Dar es Salaam, Tanzania. www.watercomtz.com, Email:info@watercomtz.com